# *Ile Ishara*

Asante.

Naamini.
Bwana, naamini; Bwana, naamini,
Mambo yote yawezekana; Bwana, naamini.

2 Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi, na katika uchaji huu wa wakati huu, tukijua kwamba tumekusanyika tena, tumekutanika hapa katika Jina la Bwana, kumwabudu Yeye. Sijui, katika kusanyiko hili, kama kunaweza kuwa na mmoja ambaye huenda ana haja maalum ambayo ungetaka kuifanya ijulikane kwa Mungu, usiku wa leo, huku mnapoinua mikono yenu kukumbukwa katika maombi. Chini katika orofa ya chini, na kwenye roshani, na kote kila mahali, vile vile tu, Yeye anaona mikono yenu.

3 Mungu mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi, tunakuja Kwako, katika Jina la Bwana Yesu. Kwa sababu, tumeahidiwa kama tungekuja katika Jina Lake, tungepata haja yetu. Kwa hiyo tunaomba, Baba, kwamba Wewe utatusamehe kwanza jambo lolote lililoko katika njia yetu, kusudi maombi yetu yangezuiliwa usiku wa leo, jalia Damu ya Bwana Yesu sasa hivi ilipie hilo, tunapokiri makosa yetu kwa unyenyekevu. Pia tunaombea kila haja, kila moja wa mikono hiyo iliyoinuliwa. Unajua kilichokuwa chini ya mkono huo, Bwana, maana yake. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utaijibu kulingana na hekima Yako kuu, Bwana, ambayo tunafahamu kwamba Wewe unajua mambo yote, na uliyajua tangu mwanzo.

4 Pia tunaomba huu utakuwa usiku ambao utakumbukwa kwa muda mrefu, kwa sababu ya Uwepo Wako kuwa pamoja nasi. Tunaposimama usiku wa leo kwenye huku Kutoa Shukrani, kumalizika kwa siku, sherehe kubwa kote nchini, ya jinsi Wewe ulivyokuwa mwema kwa babu zetu, sisi pia tunageuza vichwa vyetu kukushukuru Wewe, Bwana, kwa kile ambacho Wewe umetufanyia sisi. Sasa tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia mambo haya yote tunayoomba, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo, na kwa heshima Yake. Amina.

Mwaweza kuketi.

5 Kwa kweli ninashukuru kwa majaliwa ya kuwa mahali hapa tena, usiku wa leo, tumekusanyika katika ukumbi huu wa Maskani ya Uzima, kuwanenea watu.

6 Tunasikitika. Ndugu Moore alisema walikuwa hawajawahi, katika historia ya kanisa, kuwa na watu wengi sana. Wamewarudisha wengi, usiku wa leo, kuliko walivyowahi kufanya katika historia yote ya kanisa, kutoka mbele huko

nje. Kila mahali pamejaa ndani, nje, orofa ya chini, kuzunguka kuta, na kwenye ushoroba na nje barabarani, na bado watu wanakuja. Kwa hiyo tunashukuru kwamba kungali na njaa ya kusikia Neno la Mungu, na sasa tunashukuru kwa hili.

7 Na sasa, Bwana akipenda, kesho usiku huenda tukaanza kuwaombea wagonjwa, kama vile huwa tunakuwa na siku moja ama mbili usiku, tukiwa hapa kwenye mikutano hii, ambazo tunawaombea wagonjwa. Naye Bwana kwa kweli amekuwa akitubariki hivi majuzi kwa mambo hayo.

8 Nilikuwa nikiwaambieni asubuhi ya leo kuhusu mke wangu, na jinsi ambavyo sasa kwa karibu miaka mitatu, karibu, loo, miaka mitano au sita iliyopita, kwa kumshika mkono usiku mmoja (nikijaribu kumwonyesha mtu mwingine, mwanamke mwingine, kile mtetemeko . . . ), nikijua hakuwa na shida yoyote, nilimkuta akiwa na kivimbe. Daktari asingeweza kukipata. Miaka mitatu au minne ikapita, asingeweza kukipata.

9 Hatimaye kikaonekana, yapata miaka miwili iliyopita, kikaanza kukua upesi; kutoka kwa ukubwa wa jozi, ukubwa wa limau, sasa kufikia ukubwa wa balungi. Tabibu . . . Tulikuwa tunashikilia, kwa imani. Naye tabibu akasema, "Lazima tu ukiondoe. Kitageuka kuwa cha kufisha. Huna budi kufanya hivyo."

10 Basi jana, au siku moja kabla, nikijua kuwa jana alikuwa aende kwa ajili ya mwisho wake. Kabla ya uchunguzi huo, nilipiga magoti chumbani, nikiomba, moyo wangu wote. Ndipo nilipoinuka, au kuanza . . . Kabla sijainuka, Yeye aliniambia jambo la kusema. Ndipo nikasimama. Naye daktari hawezi kupata dalili yake, popote. Chote kimetoweka. Na—na kimetoweka kabisa, wala hakipo tena.

11 Nikampigia simu tena, muda mfupi uliopita, naye alikuwa na furaha sana. Akasema, "Juma lililopita," kasema, "Bill, maumivu yalikuwa mabaya sana, hata nisingeweza kuketi kwa utulivu, nisingeweza kulala usiku, wala chochote." Kasema, "Kila wakati nilipojaribu kupinduka, kivimbe hicho kikubwa kikapinduka ndani." Ndipo kasema, "Ninayo maneno kwa daktari hapa, kasema, 'Bibi Branham . . . '" Punde tu alipokuja kutoka kwenye meza, yeye na dada wengine. "Kasema, 'Hakuna dalili hata moja. Sijui ni nini kilichofanyika.' Kasema, 'Hakuna dalili hata moja.' Na yeye akasema-akasema, 'Simama.' Na kile alichosema nifanye, nilikifanya. Na, hilo, Bwana aliyajibu yaliyobaki."

12 Ninatazama hapa chini juu ya rafiki yangu wa kale. Si muda mrefu uliopita, rafiki jina lake ni . . . Yeye ni Mjerumani. Jina lake ni D-a-u-c-h, nafikiri, jinsi anavyoliendeleza jina lake. Lakini sisi humwita Dauch, maana siwezi kulitamka hilo neno la Kijerumani vizuri. Mwenye umri wa miaka tisini na moja. Nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, muda si mrefu uliopita.

Mtu mwema, aliyekuwa msaada mkubwa kwa Oral Roberts na wengine wengi. Lakini alipokuja siku moja kwenye maskani. Hakuwa na mavazi; alitaka kubatizwa, hata hivyo.

13 Hivi majuzi, alikuwa na umri wa miaka tisini na moja. Si tu kwamba alikuwa na mshtuko wa moyo, bali kusita kabisa kwa moyo. Mke wake aliyeketi pale, ni mwuguzi msajiliwa wa muda mrefu aliyehitimu. Walimpeleka hospitali huko Lima, Ohio, pamoja na baadhi ya madaktari maarufu kuliko wote waliokuwa nao nchini. Hakuna nafasi kwake kuishi saa moja au zaidi, alikuwa amekwisha; kusita kwa moyo, umri wa miaka tisini na moja, na mshtuko wa moyo. Nikawaza, "Maskini Ndugu Bill Dauch, labda kumwona mara yangu ya mwisho. Lazima nijaribu kumfikia." Niliomba usiku kucha. Wakati waliponiambia alikuwa amelazwa na kusita kwa moyo, nilijua, kwenye umri wa miaka tisini na moja, asingeweza kutoka.

14 Kwa hiyo, rafiki yangu mwema namna hiyo sasa, na wa familia yangu, ndipo nikaondoka kukutana na yeye, asubuhi iliyofuata. Njiani nikienda, nilikuwa nikiwazia, "Jinsi alivyokuwa mtu mwema!" Ndipo nikawaza, "Siku moja nitamwona tena." Basi nikaingia ndani ku . . .

15 Niliendesha motokaa kwa kasi, na nikawa na kuchanika kwa tairi, hata sikuwa na wakati wa kuifanya isawazishwe au kuchukuliwa . . . Gurudumu hilo lilikuwa nje ya usawa, lilichanua tu tairi vipandevipande, nikikimbia katika barabara hizo za saruji. Ndipo nikaingia ndani, nikasema, "Sina wakati kabisa wa kubadilisha hiyo."

16 Mtu huyo akasema, "Utaipasua, katika maili zingine mia mbili."

17 Nikasema, "Sina tu wakati, bwana. Asante. Acha tu ipasuke." Tena nikasema, "Nina tairi ya akiba. Inanibidi kumfikia rafiki anayekufa."

18 Ndipo nikaanza kutembea kuzunguka pale. Na nikatazama juu, na kukaja ono. Nikamwona Ndugu Dauch ameketi kanisani. Nikamtazama, akija, na hapa akaja kuteremka mtaani, na kushika mkono wangu na kuutikisa. Akasema, "Nenda kamwambie, 'BWANA ASEMA HIVI.'"

19 Huyu hapa ameketi, bwana. Na karibu ibada iliyofuata, ilitokea kwamba nilitazama hapo chini, na hapo ameketi Ndugu Dauch ameketi kanisani, ameendesha motokaa maili mia tatu kutoka Ohio. Nilienda New York juma lililopita, hapo aliketi huko New York, moja kwa moja kati ya hayo yote. Yeye huyu hapa chini Shreveport, usiku wa leo, ameketi hapa sasa.

20 Ninapopitia malango makubwa ya wakati, kuingia Umilele, kama Mungu akiniruhusu nipite kwa amani, siku moja nitapeana mkono na yeye upande ule mwingine, maana ni Mungu yule yule.

21 Siku chache zilizopita, mambo makuu, siwezi tu kuingia kuwaambieni ni mambo gani hasa yaliyotendeka katika siku chache zilizopita. Inaonekana kana kwamba, ninaamini, katika ninii ya mwisho. . .tangu tukio lile kule Colorado, majuma machache yaliyopita, Bwana amekuwa wa neema zaidi kwangu, ku—kujibu maombi. Na kunapaswa kuwa na hatua ya tatu, mwajua, ya huduma; nami siwezi kueleza, kwamba ni kitu gani. Na kwa hiyo ninaamini Bwana yu pamoja nasi na anaenda kufanya mambo makuu.

22 Usiku wa leo, nilifikiria, kwa kuwa hii ilikuwa ni sherehe ya kutoa shukrani, badala ya kuhubiri, ningechukua tu kama somo la shule ya Jumapili, na kuweka msingi kwa ibada ambayo. . .ama ibada ya uponyaji na i—ibada yoyote, msingi wa Injili. Na nilimfanya ndugu kusoma kutoka katika Kitabu cha Kutoka, mlango wa 12. Ninaenda kuendelea kusoma ninii. . . ama kusoma tu kutoka pale kifungu kingine ambacho alisoma, tena. Ningependa kurudi kupata wazo langu. Kifungu cha 12 cha mlango wa 12, na kifungu cha 13, nafikiri ndivyo.

> *Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huu, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi Bwana.*
>
> *Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile* nyumba *mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu,* lisiwapate *pigo lolote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri.*

23 Hayo ni Maandiko ya kipekee kwangu mimi. Na sasa nina Maandiko mengi, mengi hapa niliyoandika, na muhtasari, ambao ningetaka kuzungumza kwa dakika chache kutoka kwao. Na nisingeninii. . .kujaribu tu kulifanya kama somo la shule ya Jumapili, ili kwamba tutaelewa dhahiri.

24 Na ninatazamia wakati wa kutokea, kwa Roho wa Mungu, katika siku hizi za mwisho tunazoishi ndani yake sasa; kwa mfuriko mwingine wa Roho Mtakatifu, ndani ya Kanisa; kwa ajili ya imani ya kunyakuliwa, kabla tu hakujaja. Na kila kitu kimekaa sawasawa kwa ajili ya hilo. Pia ninaamini kwamba sasa tuko kwenye wakati ambapo Neno linapaswa kuwa na utangulizi. Ninaamini kwamba wakati wa kuweka kando kanuni zetu za imani na mawazo yetu, na kurudi kwenye Neno.

25 Mungu, katika kila kizazi, kama nilivyozungumza jana jioni, Yeye alizungumzia mwisho tangu mwanzo. Alisema kile ambacho kingekuwa katika kila kizazi. Pia, tena, "Mungu, katika nyakati mbalimbali, Yeye aliwatuma manabii." Wakati kila majira yalipowadia kwa mambo hayo kutendeka kwa wakati huo, Yeye aliwatuma manabii. Nalo Neno la Bwana daima huwajia manabii Wake, nabii wa wakati huo. Na

kila wakati, jambo pekee nabii huyo alifanya lilikuwa ni kudhihirisha, hasa, ahadi kwa ajili ya wakati huo.

26 Ndipo wakati Bwana wetu Yesu alipokuja jukwaani, Yeye alikuwa ni dhihirisho la Neno la wakati huo. Alikuwa ni Isaya 9:6, "Kwetu amezaliwa Mtoto," na kadhalika. Na tena Yeye alikuwa pia Isaya 35, Isaya 28:19, yeye yule. Hayo, Maandiko hayo yote yaliyotabiriwa, Yeye alikuja kudhihirisha hilo Neno. Alifanya hasa kile kilichopaswa kufanywa katika siku hiyo. Kwa kuwa, Neno, Kitabu hiki ndicho Neno, nalo Neno ni Mungu.

27 Na sasa imewekwa tayari. Inahitaji tu mtu fulani ajitokeze jukwaani, kudhihirisha ahadi hizo, imani katika wi—wito wa Mungu. Nami ninajua tumepitia uigaji mwingi, na kadhalika. Musa na Haruni walikabiliana na jambo lilo hilo. Bali, hilo likitokea, simama kimya. Musa, wakati alipokabiliana na hao wenye ufahamu wa kiakili, aliwaacha tu waende. Walikuwa wanafanya hasa kile alichofanya, lakini yeye alingojea mpaka madhihirisho kamili yakafanyika. Na imeahidiwa jambo lile lile litatukia katika siku za mwisho. "Kwa kuwa kama Yambre na Yane walivyompinga Musa," ndivyo watakavyofanya watu wa siku hii. Bali, sasa, hiyo haikomeshi ahadi. Hiyo itakuza tu ahadi. Hiyo itaifanya halisi.

28 Sasa ninataka mwone, usiku wa leo, kile tunachoenda kuzungumzia ni: *Ile Ishara*. Ishara!

29 Sasa, kwanza, ninataka mwone kile—kile utaratibu wa hii ulicho, utaratibu wa Pasaka. Lazima iwe ni kondoo dume, na lazima achunguzwe kwa siku kumi na nne.

30 Ni mfano mkamilifu jinsi gani wa Kristo, kitu halisi, Mume, Mwana-kondoo, na Yeye alichunguzwa kwa miaka mitatu na nusu ya huduma Yake, kupitia wakosoaji na kila kitu, makasisi wa siku hiyo, bali alithibitishwa kushikilia imara Neno la Baba. Hata mbele za Shetani, Yeye alisema, "Imeandikwa. Imeandikwa." Kila mara Yeye alimshinda adui, juu ya Neno.

31 Mfano mkamilifu kwa ajili yetu leo hii, kumshinda adui daima kwa Neno la Mungu ambalo limeandikwa kwa ajili ya siku hii!

32 Ndipo Yeye akawaambia, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Kwa maneno mengine, "Kama sifanyi kile Maandiko yanachosema kinapaswa kufanywa katika siku hii, basi mimi ni asiyeamini. Lakini basi ni nani awezaye kunihukumu Mimi kuwa nina dhambi?" *Dhambi* ni "kutokuamini." Yeye alidhihirisha kila ahadi ambayo Mungu alitoa kwa ajili ya siku hiyo. Aliitimiza. Alitimiza siku hiyo kwa sababu Yeye alikuwa ndiye Masihi, na hiyo ilikuwa ni siku ya Masihi.

33 Sasa tunaona kwamba, wakati wa jioni, mwana-kondoo aliuawa, baada ya chakula cha jioni, i—ikielekea mwisho wa jioni. Vile vile tu Mwana-kondoo alivyouawa!

34 Sasa tazama, kusanyiko lote la Israeli iliwabidi kumwua mwana-kondoo. Pia ni Israeli walioshuhudia kwa ajili ya kifo Chake na kulilia Damu Yake. Tutazungumza juu ya hilo kesho usiku, kama Bwana kwa uwe-. . .ikiwezekana na kumpendeza Bwana, "Damu mikononi."

35 Tena angalia, damu hii haikuchanganywa na chochote kingine. Isingeweza kuchanganywa. Ilikuwa tu ni damu, pekee, ya mwana-kondoo yule. Na haina budi kupakwa juu ya kizingiti na mwimo wa mlango. Isingeweza kuchanganywa.

36 Hiyo ndiyo leo hii, wanajaribu kuchanganya kila kitu leo hii na Hili, kanuni za imani na mashirika, na—na kila namna ya burudani na kila kitu, bali halitachanganyikana! Hapo ni yakini, Hilo halitachanganyikana na chochote. Damu isingechanganyikana.

37 Pia haina budi kuliwa, tayari, watu waliovaa tayari kwa safari. Hii ilipowekwa, watu lazima wawe tayari kwa ajili ya safari.

38 Si kwa ajili ya asiyeamini, aliyesimama nje na kuhurumia Hilo. Ni kwa ajili ya mwaminio ambaye tayari yuko chini ya Damu, amevaa tayari, viatu miguuni, fimbo mkononi mwake, viuno vyake vimefungwa, na tayari kwa safari.

39 Sababu ya kuchagua siku hii, siku ya shukrani, sherehe, kwa sababu ni she—sherehe leo, ambayo babu zetu wasafiri ambao Mungu aliwabariki kuja huku kuanzisha taifa. Na wakaanzisha, na taifa lenye nguvu. Linasimama juu ya kila kitu ulimwenguni leo, katika ufisadi wake wote, bali halina budi kuanguka. Halikuwahi kuwa kubwa, kulingana na Maandiko. Halikuzeeka kamwe. Lilikuwa kijana, mwana-kondoo. "Ndipo mwana-kondoo akanena kama joka aliyekuwa mbele yake." Liliinuka si kutoka kwenye maji, wingi na umati wa watu, bali liliinuka kutoka katika nchi kavu. Kwa hiyo tunaona kwamba mwana-kondoo alikuwa na pembe mbili, ambazo zilikuwa ni uweza wa kisiasa na wa kidini; bila shaka, wanaenda pamoja sasa kunena kama joka, kuunda alama ya mnyama, na bado tunao uhuru wa kumwabudu Mungu katika taifa hili.

40 Na sasa tunainamisha vichwa vyetu, kuzunguka meza yetu leo hii, kumshukuru Mungu kwa chakula cha kimwili ambacho Yeye amekiotesha kwa ajili yetu na kutuandalia, mwaka huu. Na kama hakuwa amefanya hivyo, tungekuwa sote tumekufa. Kwa sababu, njia ya pekee unayoweza kuishi kimwili, ni kwa sababu inabidi kitu fulani kufa kila siku ili uweze kuishi. Kama ukila nyama ya ng'ombe, ng'ombe alikufa. Ukila kondoo, vema, alikufa. Ukila viazi, uhai wake, ulikufa. Ukila mboga za

majani, zilikufa. Unaishi tu kwa kitu kilichokufa. Na kama kitu hakijakufa, huwezi kuishi.

41 Na kama inabidi kitu fulani kufa, ili uweze kuishi kimwili, ni zaidi sana jinsi gani kwamba kitu fulani ilibidi kife ili tuweze kuishi Milele. Na ni kwa kiini cha kifo hiki ninachozungumzia usiku wa leo, ambapo tuko hai usiku wa leo. Kitu fulani hakina budi kufa. Pasaka ilikuwa ni mfano wa Kristo, Uzima wetu wa Milele. Sasa tunataka u—usikivu wenu mkamilifu.

42 Ishara. Alisema, "Damu itakuwa ishara kwenu," a—alama. "Ishara," kulingana na Webster, "ni ushahidi wa gharama ambayo imelipwa." Ishara ni ushahidi kwamba gharama imelipwa.

43 Kama vile kampuni za usafiri wa gari la moshi na kampuni za mabasi. Unaingia na unataka kuwa na . . . Unasafiri tu kwenye basi kwa ishara katika sehemu nyingi, au gari moshi. Unanunua nauli yako, unailipia, na wanakupa tikiti kwamba nauli yako imelipwa tayari. Kwa hiyo hiyo ndiyo inayokubidi kuwa nayo kwenye gari la mtaani au kampuni ya gari la moshi.

44 Mwana-kondoo wa Israeli, aliyechinjwa, ndiye aliyehitajika na Yehova. Ili kuepuka kifo, lazima kuwe na kifo mbadala. Naye Yehova alihitaji mwana-kondoo alyechinjwa, na damu ilikuwa ishara kwamba matakwa yalikuwa yametimizwa. Sasa, damu ilikuwa—ilikuwa ni ishara kwamba kitu fulani kilikuwa kimekufa, nayo damu yenyewe ilikuwa ni ishara. Ilikuwa inasema, kwamba, "Nyumba hii imetimiza matakwa ya neno la Yehova, na kwa hiyo inalindwa na ishara hii, kwamba nauli yetu imelipwa."

45 Ni mfano wa kupendeza jinsi gani hapa, aliyo Kristo kwa hii, ni mfano jinsi gani wa Ishara yetu ya leo!

46 Uhai ulitoka kwa kafara. Na sasa damu ilikuwa ndiyo ishara, maagizo Yake yalikuwa yametekelezwa. Damu! Haikumbidi Yehova kukuona ukimwua mwana-kondoo. Ulikuwa tu na damu juu ya mlango wakati malaika wa mauti alipopita, na hiyo ilikuwa ni ishara kwamba mwana-kondoo alikuwa ameuawa. Damu ilikuwa ndiyo ishara ya kwamba matakwa ya Yehova yalikuwa yametimizwa katika nyumba hii, na kwamba gharama ilikuwa imelipwa, na ishara ilikuwa ni hiyo. "Nionapo ishara, nitapita juu yenu." Ishara ikiwapo, ilionyesha gharama. Unaona, damu haikuwa ndiyo kifo, bali ilikuwa ni ishara ya kifo. "Nionapo damu, nitajua gharama ya kifo imetimizwa, kwa hiyo nitapita juu yenu."

47 Tazama, unaona, mwabuduo aaminiye alitambulishwa na sadaka yake, kwa ishara. Mwabuduo aliyemwamini Yehova, na alikuwa ametimiza matakwa ya Yehova, alikuwa amejitambulisha mwenyewe kwa kuweka ishara kwake mwenyewe na kwa nyumba yake, hiyo ilikuwa, mwabuduo aliamini hiyo. Mfano mkamilifu wa Kristo wa siku hii!

Ndipo, damu ilikuwa ni ishara ya utambulisho, kwamba huyu mwaminio tayari ametimiza matakwa ya Yehova. "Nami nina hakika malaika wa mauti itambidi apite mbali na nyumba yangu, kwa sababu nimetimiza ishara ya Yehova. Mwana-kondoo ameuwa, badala yake, kwa ajili ya familia yangu na wapendwa wangu walio chini ya damu hii, na hiyo hapo ishara kwamba mwana-kondoo amekufa." Amina. "Hiyo hapo ishara. Matakwa ya Mungu yametoshelezwa." Amina. Nikiwazia juu yake, moyo wangu huruka kwa furaha.

48 Sasa, uhai wa mnyama usingeweza kurudi juu ya mwaminio, kwa hiyo basi damu ilibidi isimame kwa ajili ya ishara. Unaona, damu, iliyofungiwa ndani ya mnyama ambayo ilianzishwa kutoka kwa seli moja ya damu, ilikuwa imefanya damu hii yote iliyokuwa ndani ya mnyama. Damu hii ilipotawanywa, uhai ulitoka ndani ya huyo mnyama. Sasa, mwabuduo, akijitambulisha mwenyewe na damu, ilimbidi kuonyesha kemikali halisi ya damu. Kwa nini? Hiyo ndiyo yote aliyoweza kuonyesha. Kwa sababu, uhai wa mnyama usingeweza kurudi juu ya mwanadamu, kwa sababu uhai wa mnyama hauna nafsi. Lakini mwanadamu anayo nafsi. Hivyo basi uhai usingeweza kurudi, kwa hiyo damu ilibidi isimame kwa ajili ya ishara ya kifo.

49 Sasa tunayo Ishara katika siku hii. Tumepewa Ishara ambayo ndiyo halisi iliyoonyeshwa na ule mfano. Kwa ishara hiyo ya kawaida, tumepewa ya Kimbinguni, Ishara kuu. Yote yaliyofananishwa na hiyo kwa njia ya kivuli yamepewa kizazi hiki, kimepewa Ishara. Sasa tunaye Roho Mtakatifu, ndiye Ishara yetu, na Hiyo ndiyo utambulisho wetu kwamba tumekubali kifo cha Mwana-kondoo. Siyo tu kwamba Yesu alikuwa ni uhai wa mwanadamu kurudi juu yetu, bali Huo ulikuwa ni Mungu Mwenyewe aliyedhihirishwa katika mwili, aliyerudisha juu yetu kufanywa wana wenye mamlaka, kwamba sasa tu wana na binti wa Mungu. Hiyo ndiyo Ishara. Ni utambulisho wetu wa pasaka. Ni utambulisho wetu kwamba tumemwamini Mungu, na Mungu amekubali.

50 Huko nyuma hawakuwa na Injili kama tulivyo nayo leo hii, ilifundishwa katika desturi na ikapitia kanuni, kwa sababu Roho Mtakatifu hakutolewa.

51 Lakini, leo hii, tuna Kitu halisi. Hatuna desturi tu, ama kemikali tu; usingeweza kuchukua Damu ya Yesu Kristo na kuipaka kwa kila moyo. Bali Mungu alimtuma Roho Mtakatifu arudi, hiyo ndiyo Ishara iliyokuwa juu ya mwanadamu, ndani ya moyo wa mwanadamu. Na huo ndio utambulisho wako kwamba umekubali mpango wa Mungu, ukatimiza matakwa ya Yehova; Yeye alikutimizia hayo pale Kalvari, na wewe umeyatimiza juu ya magoti yako. Na Mungu amekupa alama ya Ishara, kurudi kwa Roho aliyekuwa juu ya Kristo, yuko ndani yako, na utambulisho wa hakika wa maisha Yake, kifo, kuzikwa, na

kufufuka, na yu hai milele, sasa ndani ya Kanisa linaloamini. Amina. Ni Ishara ya kweli, alama ya ishara. Hiyo inaweza . . .

52 Itanenewa maovu, hakika. Hiyo ndiyo sababu yake kuwa hapo. Misri iliidhihaki, vivyo hivyo na watu leo hii. Lakini bado ni Ishara inayotakiwa na Mungu. Wasingeweza kuweka damu, Damu kemikali ya Yesu juu ya, kama walivyofanya mwana-kondoo; kwa sababu waliweka damu kemikali ya mwana-kondoo juu yake, kwa sababu hakukuwa na uhai ndani ya mwana-kondoo ulioweza kurudi juu ya mwabuduo. Lakini hapa Uhai uliokuwa katika Damu . . . Ambayo, "uhai uko katika damu." Sasa Damu ilimwagwa pale Kalvari, ikalowesha nchi, nasi tunayo Ishara ya Damu, ambayo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, kututambulisha kama waaminio.

53 "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," si tu wanaokiri, bali waaminio waliotambulishwa! "Huenda zisifuate. *Labda* zitafuata. *Huend*a zitafuata"? Yesu alisema, "Zitafuatana na hao waaminio." Haiwezekani tu kabisa hilo kukosa kufanyika! "Kazi nizifanyazo nanyi pia mtazifanya." Huo ndio utambulisho. Utambulisho wa Yesu ulikuwa ni kudhihirisha Neno la Mungu, ambalo Yeye alikuwa. Na utambulisho wa Kanisa leo hii ni kudhihirisha Neno lililoahidiwa la siku hii, kwa Roho yule yule aliyelidhihirisha na kulihuisha Neno wakati ule. Roho yuyo huyo hulihuisha Neno kwa mwaminio leo hii na kudhihirisha kitu kile kile, akionyesha kwamba Ishara iko juu ya mtu huyu, ambayo ni Uzima uliofufuka wa Yesu Kristo akiishi ndani ya mwaminio Wake. Loo, hiyo yafaa kuliwasha moto kanisa! Na hiyo ni kweli, kweli tu kama iwezavyo kuwa.

54 Lazima tujitambulishe wenyewe na Sadaka yetu. Lazima tutambulishwe katika kifo Chake. Wakati Myahudi alipoweka mkono wake juu ya sadaka, alikuwa anajitambulisha mwenyewe, akihamisha dhambi zake hadi kwa sadaka yake, ndipo sadaka ikafa. Sasa tunaweka mikono yetu, kwa imani, juu ya Yesu Kristo, na tunatambulishwa na Yeye katika kifo Chake.

55 Sio tu katika kifo Chake, lakini, ikiwa tumekubalika, tunatambulishwa si tu katika kifo Chake bali katika ufufuo Wake. Kwa Uhai uliokuwa ndani Yake, unatumwa kurudi juu ya mwaminio, kama ishara, kumbukumbu kwamba kifo kimepita kutoka kwake, na Mungu amekutia muhuri katika Ufalme wa Mungu hadi siku ya ukombozi wako. Waefeso 4:30.

56 Injili halisi ya kweli, safi kama ninavyoijua! Ninajua ni kweli. Nimeijaribu. Hakuna itikadi yoyote nyingine, hakuna uchochezi, hakuna—hakuna hila, hakuna ujanja, hakuna chochote. Ni imani safi tu isiyoghoshiwa katika Neno la Mungu na kazi zilizokamilika ambazo Mungu alihitaji pale Kalvari,

akijua kwamba hakuna kitu tungaliweza kufanya kujiokoa wenyewe. Tunakubali tu kile Yeye alichotufanyia.

57 Ibrahimu alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake kuwa mwenye haki. Ndipo Mungu akampa muhuri ya tohara, kama ishara kwamba Yeye alikuwa ameipokea imani yake. Hiyo hapo Injili.

58 Sasa wakati tunapodai kwamba tunamwamini Mungu, basi Mungu ataitambulisha imani yetu, kwa kutupatia Ishara ya Damu ya Yesu, aliyetumalizia kazi pale Kalvari, ndipo Uhai wetu uko ndani ya Wake. Uhai wa Sadaka yetu uko ndani yetu.

59 Usingeweza kuja kwa damu ya kemikali ya mwanakondoo, kwa sababu hakukuwa na kitu pale cha kurudi, kemia tu. Usingeweza kuhamisha damu hiyo kuiweka ndani ya mwanadamu. Haitafanya kazi, damu ya mnyama haiwezi kuingia ndani ya damu ya mwanadamu. Kwa hiyo kemikali zisingefanya kazi, kuonyesha kwamba ilikuwa ni kivuli kilichoonyeshwa kimbele.

60 Lakini sasa Uhai ule uliokuwa katika Damu unakuwa ndiyo Ishara. Na sasa wakati tunapojitambulisha wenyewe katika kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, kwa kumwamini Yeye na kubatizwa katika kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Tunapoinuka, Roho Mtakatifu yupo pale kutupatia Ishara, Ishara ya Milele iliyoandikwa katika moyo wako, nafsi, umbile, nia, mwili, kila kitu kingine, kwamba wewe ni mtu aliyetengwa, kutokana na kutokuamini. Wewe ni mtu aliyetengwa, kutoka kwa mambo ya ulimwengu. Umetengwa na mauti. Umetengwa na kila kitu. Na wewe ni bidhaa ambayo Mungu ameitia muhuri katika Ufalme, kwa Roho Wake Mtakatifu.

61 Hakuna ibilisi, hakuna—hakuna ugonjwa, hakuna mauti, hakuna huzuni, wala chochote kingine, kiwezacho kukusumbua mradi tu unashikilia hiyo Ishara juu yake. Amina. Imani yako isiyobadilika hudunda hivyo, nayo huumba sura ya Yesu Kristo, ile Sura unayotembelea leo hii.

62 "Na nitakapoona ile ishara, nitapita juu yenu." Ni ishara, ni ishara ya kwamba gharama imelipwa. Yesu alilipa gharama, na wewe uliipokea kutoka Kwake. Ukishikilia Ishara mkononi mwako, unalo hakikisho la ufufuo. Unalo hakikisho kwamba kila kitu unachohitaji, katika safari hii, kinapatikana katika hiyo Ishara ya kuteswa Kwake Kalvari, ambapo alilipia gharama ya kila laana ambayo ingeweza kuwekwa juu yako. Ishara hiyo hunena amani. Amina.

63 Hakuna ibilisi awezaye kusimama mbele Zake. Hakuna kitu kinachoweza kusimama mbele Zake, kwa sababu Mungu amekubali Hiyo. Na wewe unashikilia Ishara mkononi mwako, kwamba gharama imelipwa. Loo, ni—ni Ishara chanya.

64 Mnajua, katika mahakama, kesi ikiwekwa, wakati unajua kwamba ulikuwa unakabiliwa na kifo, kama huyu hapa mtu

wa vilabu vya usiku ambaye ndiyo kwanza amwue huyu Bw. Oswald. Kama ulijua ulikuwa unakabiliwa na hicho, au kitu sawa na hicho, ungekodi wakili bora kuliko wote uwezaye kumpata.

65 Ningefanya hivyo. Kama nilijua maisha yangu yalikuwa hatarini, ningemkodisha wakili bora kuliko wote niwezaye kumpata. Kila mtu angefanya hivyo. Ndilo jambo la pekee lenye maana kufanya.

66 Sasa, katika kisa hiki, kujua kwamba unaenda kwenye kiti cha umeme, na unaenda kutengwa na familia yako, milele, kwa kuwa wanaenda kukuua kwa umeme, ama chochote kile, kwa sababu unajua una hatia. Naye wakili huyu anajaribu kuitetea kesi yako.

67 Sasa wakili anaweza kuwazia kwamba ameweka yote chini. Lakini, unaona, ni hakimu gani anaenda kuamua kesi, hata kama wakili anaweza kuiweka wazi kwake kwamba umehalalishwa katika kitendo chako. Wakili hana budi kuiweka waziwazi kwa hakimu, ili hakimu aweze kuona haki katika tendo lako.

68 Ee Mungu, laiti watu wangeweza tu kuona hili! Hakimu wetu ndiye Wakili wetu. Kesi imeisha. Imeisha. Yule yule aliye Hakimu ndiye Wakili, ndiye Wakili wetu. Kesi imeisha, tunayo Ishara. Hakimu na Wakili pia ni Mtu yule yule. Wakati Mungu alipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Hakimu wetu akafanyika Wakili wetu, na kesi imemalizika. Na Roho Mtakatifu yupo hapa kwa ajili ya Ishara kwamba tuko tayari kupita kutoka hapa kuingia katika Nchi za ng'ambo.

69 Tuko huru kutokana na dhambi; si wa dhambi tena, si wa ulimwengu. "Watoto wadogo, nyinyi si wa ulimwengu." Hakimu wetu na Wakili alikuwa ni yule yule, Mtu yule yule, kwa hiyo kesi imemalizika. Ke—ke—ke—kesi ilikuwa kubwa sana dhidi yetu! Kesi, kwamba tulikuwa tumetenda dhambi, ilikuwa kubwa sana dhidi yetu, mpaka si hata Malaika mkuu angeweza kuitetea; asingeweza kutimiza masharti. Hakuna Malaika, hakuna Kerubi, hakuna Serafi, hakuna kitu kingaliweza kutimiza gharama. Kitu cha pekee kingaliweza kufanywa kuokoa jamii ya binadamu kilikuwa ni kwa Hakimu kuchukua mahali na kufanyika Wakili, pia. Na hicho hasa ndicho Yeye alichofanya.

70 Kama ishara, au damu, katika wakati wa kutoka Misri, kutoka kwao, kama ishara ilikuwa ndiyo alama kuu, sasa ikiwa . . . Ishara haikufaa kitu isipokuwa iwe ishara iliwekwa hadharani. Ilibidi ishara iwekwe hadharani. Sio mtu wa kuiunga mkono ishara; bali ishara lazima iwekwe kazini!

71 Na haijalishi ni kiasi gani mtu yeyote angalithibitisha kwamba alikuwa ni Myahudi, na Myahudi wa agano, kwa tohara, hiyo haikufanya chochote kuhusu hiyo hata kidogo.

Ninii...Ilihitaji ishara, si agano. Yeye kamwe hakusema "nionapo alama ya agano." Bali, "Nionapo ishara!"

72 Kwa hiyo, leo hii, huenda ukawa na madai ya kuwa Mkristo, huenda ukawa agano, pamoja na agano na Kristo; bali isipokuwa Ishara hiyo iwekwe wazi katika saa hii ya mwisho tunaokaribia sasa, hakuna njia Kwake kupita. Ishara lazima ionyeshwe wazi. Lazima iwekwe.

73 Sasa, kumbukeni, Myahudi angeweza kujitokeza na kusema, "Nitawachukua kando enyi wanaume. Ninaamini hilo kuwa kweli. Ninamwamini Musa, nabii. Ninaiamini hiyo Nguzo ya Moto inayomwongoza. Ninaamini huyo ni Yehova." Unashuhudia yote ya hilo, unaamini Neno lote, ujumbe wote, lakini hata hivyo unasema, "Sasa mimi niko sawa tu kama wewe, kwa sababu mimi ni Myahudi aliyetahiriwa." Kama hakuwa na damu hiyo kwenye usiku wa pasaka, alikufa hata hivyo.

74 Na leo hii, kila kanisa, kila mtu binafsi, ambaye sivyo na hawezi kuonyesha Ishara hiyo, ya Roho Mtakatifu, anakufa kiroho na atakufa. Haijalishi ni kiasi gani unaamini katika kifo, kuzikwa, na kufufuka; haijalishi ni kiasi gani unaweza kurudia Kanuni ya Imani ya Mitume, kuirudia, au chochote uwezacho kufanya; haijalishi jinsi ulivyoelimika vizuri, na ni ujuzi gani wa kitheolojia umekuwa nao; huenda ukawa na shahada ya udaktari, na Shahada ya Kwanza ya Sanaa, na chochote kingine, DD, LD, Daktari wa Kilatini, au chochote kile uwezacho kuwa, au fasihi, lakini hiyo haitaifanya. Lazima kuwe na Ishara iliyowekwa wazi.

75 Ilikuwa tu ni kivuli cha iliyo Halisi kwa ajili ya siku hii, Kitu halisi kilichofananishwa. Ishara lazima ionyeshwe. Myahudi angeweza kutoa, angeweza kutoa thibitisho kwamba yeye alikuwa ndani ya agano; lakini kama ishara haikuwepo, agano halikufanya kazi. Na ndivyo ilivyo leo, ndugu yangu, dada yangu.

76 Ninawatakeni mkumbuke hili. Nyinyi mlio ndani, nje, kwenye orofa ya chini, popote ulipo, saa imewadia. Na kila mtu anaweza kuona ubutu wa kanisa leo hii. Kila mtu anaweza kuona kupooza kwa wengi, wengi sana wa washiriki. Ni kwa sababu kwamba mmecheza, mmechukua misisimko na mmechukua mambo mengine. Pia mmetumaini juu ya hekima ya mwanadamu fulani, juu ya theolojia ya dhehebu fulani, juu ya kuwa mshiriki wa kanisa la mama yako, na juu ya mchungaji fulani mwaminifu. Lakini yote ni mambo mazuri, sina kitu dhidi yao, si zaidi ya jinsi tohara ilivyokuwa kwa Myahudi, bali hiyo haikuwa ni mpango wa Mungu. "Nionapo damu," na hiyo pekee!

77 Basi leo hii Roho Mtakatifu ni agano la Mungu na watu wa Mungu wa agano. Roho Mtakatifu, Uhai wa Kristo aliyefufuka, hauna budi kuwekwa hadharani kanisani miongoni mwa watu, ukimfanya Yeye "yule yule jana, leo, na hata milele."

78 Haijalishi wewe ni mshiriki mwaminifu kiasi gani! Huenda ukawa chochote uwezacho kuwa, mwanamume mwema au mwanamke mwema. Hilo hakika ni sawa. Tunathamini hilo. Bali Ishara pekee itakuweka hai, Ishara ya Mungu. Huenda ukawa mkufunzi wa Biblia. Huenda ukawa mtu mwema. Unaweza hata kuwa ni Rais. Unaweza kuwa chochote utakacho kuwa. Hakuna udhuru.

79 Wakati Mungu alipoanzisha kutoka katika Misri, kuita Israeli watoke kutoka Misri, kuelekea nchi Yake ya ahadi, hakukuwa na udhuru. Kila mtu ilibidi aweke damu hadharani.

80 Basi, leo hii, kutoka, ni kuitwa kutoka katika mifumo, kuingia ndani ya Bibi-arusi. Haijalishi ni kiasi gani ulivyo ndani ya mfumo, bado inahitaji ile Ishara ya Uhai wa Yesu Kristo tena. Hakuna kitu kingine kitakachofanya kazi. Bado Ishara inahitajika.

81 Kila mtu, haijalishi kama alikuwa ni mtu mwaminifu. Huenda alikuwa ndiye Farao wa Misri, naye alikuwa ndiye mtu muhimu kuliko wote wa siku hiyo, lakini ishara ilibidi kuwekwa kwake, haijalishi jinsi alivyokuwa muhimu. Kama ni askofu, kasisi, chochote kile, rais, mfalme, mwenye hekima, mtawala, hiyo haikuwa na uhusiano wowote nalo. Mungu alitambua tu watu wa agano waliokuwa na ishara. Jambo lile lile leo hii, Roho Mtakatifu atawatambua tu watu wa agano.

82 Tunakuta kwamba kifo kilikuwa tayari kuipiga Misri wakati wowote sasa. Mungu alikuwa amewaonyesha neema Yake, nguvu, na ishara.

83 Ninawatakeni mjue kwamba hiyo imefuata kila uamsho; neema, nguvu, na ishara. Neema, kuwajia watu; nguvu, kujifanya Mwenyewe ajulikane; na ishara ya wakati. Kile hasa tu alichofanya leo hii, kitu kingine. Amekifanya kwa njia nyingi. Ungeweza kuchukua Andiko hilo moja hapo na kulizungusha na kulizungusha, kwa majuma kumi hapa, na usiliache.

84 Jinsi ambavyo ingewakilisha hatua tatu ambazo tumepitia! Ingefananisha rehema tatu za Mungu, kupitia Luther Martin, na Pentekoste. . . Martin Luther, na—na pia kupitia Wesley, na Pentekoste, hatua tatu za safari. Hatua tatu za safari ya Israeli, wajumbe watatu kwa Sodoma, mambo haya yote mbalimbali ingefananisha.

85 Ingefananisha huduma ya leo. Ingefananisha ujumbe wa Billy Graham, wa neema kwa ulimwengu; wa Oral Roberts, kama nguvu kwa ulimwengu; na wa Uwepo wa Yesu Kristo, kama ishara ya mwisho kwa ulimwengu. Kwani Sodoma ilipata ishara yao ya mwisho, Kanisa la kiroho, lile liloitwa litoke, walipata ishara yao ya mwisho kabla ulimwengu wa Mataifa kuteketezwa. Yesu alisema, "Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu, jambo lile lile."

86 Ndipo tunaona kwamba mambo haya makuu yalikuwa yamewekwa wazi huko Misri, na hata hivyo shauku yao haikuwa kutubu wala kuamini ujumbe.

87 Na kama huo—na kama huo si ulimwengu leo hii, sijui ulimwengu. Wamekuwa na neema, nguvu, na kuona ishara za wakati, ishara za majira haya. Mungu akiandika, na kwa mkono Wake katika maumbile, tamasha kuu za kuogofya angani, ambazo hawajui, "vimodo virukavyo" wanaviita, na kila kitu; sputnik, na chochote kile wanachotaka kuviita, wanaanga wakiruka angani; ishara za kuogofya, mitetemeko ya ardhi, mahali mahali, bahari ikivuma, mioyo ya watu ikishindwa; hofu, kufadhaishwa na wakati, dhiki kati ya mataifa. Mambo yote ambayo Yeye ameahidi, tumeona hayo maandishi ya mkono juu ya ukuta. Tumeona kwa macho yetu.

88 Tunaona katika kanisa ambapo neema imeenenda ili kuwaita. Tunaona ambapo nguvu zimedhihirishwa na kundi la Kipentekoste, kurudisha tena ubatizo wa Roho Mtakatifu, nguvu. Pia tumeona Nguvu za kimbinguni za utambulisho wa Yesu Kristo Mwenyewe akisimama katikati yetu miongoni mwetu, na kufanya mambo ambayo Yeye alifanya hapo mwanzo. Mashahidi wale wale, hakika!

89 Israeli ikitoka, ishara tu kama ilivyo leo hii. Tazama kile Israeli walichopata katika kutoka kwao.

90 Kitu cha kwanza walichopata, kutambulisha kabisa kwamba wakati ulikuwa umewadia, alikuwa ni nabii na ujumbe. Musa alishuka akiwa na ujumbe. Neno la Mungu lilikuwa pamoja na Musa.

91 Kitu kilichofuata, ilibidi Musa atambulishwe. Naye alitambulishwa kwa Nguzo ya Moto. Hiyo ilitambulisha kazi yake, kwamba Mungu alikuwa amemtuma. Na Musa alikuwa na Neno la Mungu, hata kuumba vitu na kuvileta juu ya nchi.

92 Basi ishara ambayo Mungu aliwapatia, kwa damu, ilikuwa ndiyo utambulisho, au hakikisho, hasa, kwamba wasingeguswa katika wakati wa kifo.

93 Jambo lile lile limetendeka leo hii, jambo lile lile. Neno la Mungu limeletwa kwetu; Nguzo ya Moto iko miongoni mwetu, ikitambulisha Yesu Kristo aliyefufuka kutoka kwa wafu, "yeye yule jana, leo, na hata milele"; na hakikisho la ubatizo wa Roho Mtakatifu juu ya mioyo yetu, tukiweka upendo wetu kwa Mungu. Kutoka kunaendelea tena.

94 Israeli wakitoka, kama nilivyosema, ni mfano kama wa Kanisa likitoka, au Bibi-arusi akitoka kwenye kanisa. Bibi-arusi atakuwa ni mabaki, litakuwa ni kundi dogo, walioteuliwa, waliochaguliwa kimbele.

95 Mwanamke akiweka kipande cha kitambaa, aweke mchoro wake juu yake, jinsi anavyoenda kukikata, naye ana njia yake

mwenyewe ya kufanya chaguo. Lakini kinachosalia kutokana na mchoro huo ni kitambaa cha aina ile ile iliyokuwa kwenye huo mchoro, lakini ilikusudiwa kwake kuchukua *hiki*. Aliuandaa mwenyewe.

96 Mungu alifanya vivyo hivyo. "Nao waliosalia wa uzao wa mwanamke walioachwa juu ya nchi." Leo ni kuitwa kwa Bibi-arusi atoke kwenye kanisa, kutoka, kwa ajili ya Unyakuo. Kwa kuwa, kanisa kweli linapitia kipindi cha Dhiki kuu, kama vile nyinyi ndugu wa Kipentekoste mmelihubiri. Ninaamini hilo. Kanisa hupitia hiyo, bali si Bibi-arusi. La, bwana!

97 Mtu fulani akijadili hilo nami, si muda mrefu uliopita, alisema, "Kanisa itabidi lipitie hapo, kwa ajili—kwa ajili ya kutakaswa."

Nikasema, "Hiyo ni kweli, kwa sababu lilikataa Damu."

98 Lakini kipindi cha Dhiki kuu kikimshika Bibi-arusi, Mke Wake Mwenyewe, katika Dhiki kuu? La, bwana! Damu ya Yesu Kristo imetuosha na dhambi zote, na hakuna kutakaswa tena. Nayo Damu ya Yesu Kristo, na hiyo Ishara, kama utambulisho kwamba umetakaswa. Amina. Hiyo ndiyo Ishara ya Bibi-arusi, amevaa pete.

99 Huduma ya Musa, ya Israeli, ilikuwa ni kusanyiko lake lote lilikusanyika mahali pamoja kwa ajili ya maombi na ibada. Mambo haya yalipokuja, kama alivyokuwa akisoma usiku wa leo, iliwabidi kukaa na kushikilia. Ndivyo na kusanyiko la Bwana linavyojikusanya pamoja, kutoka kwa kila kanuni ya imani na fundisho ulimwenguni. Lilitoka pande zote za Misri, kuja mahali ambapo walikuwa wamekusanywa mahali pamoja.

100 Sisi hapa, tungeweza, tungeweza kusoma Waebrania 10:26, na kuliona wazi kabisa. Tunapoona ishara kuu za wakati wa mwisho duniani, zikituonya wakati umekaribia, tunapaswa kupendana mmoja na mwenzake kuliko tulivyowahi kufanya maishani mwetu. Kunapaswa kuwa na njaa kubwa kufika kanisani! Kunapaswa kuwa na njaa kubwa kwetu kila mmoja kumfikia mwenzake! Linapaswa kuwa ni swala la kimapenzi.

101 Siwezi kungojea kufika Tucson. Loo, Mungu alimponya maskini mke wangu! Yeye ni sehemu yangu. Ni vigumu kwangu kungojea kufika kule! Saa, ninazihesabu siku na saa, ninapoweza kufika kule kuwa pamoja na yeye.

102 Hivyo ndivyo kanisa linavyopaswa kuwa. Kuona tu hilo, Nguvu za Mungu, kile ambacho Hizo zimetufanyia, tunapaswa kuwa tukihesabu dakika, tukija pamoja katika upendo, hata tunaweza kuruka twende, siku moja, kukutana na Yesu.

103 Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, unawatisha watu, ukisema kwamba, 'Kuja kwa Bwana kumekaribia sana!'"

104 Nikasema, "Hawapaswi kufadhaika juu ya hilo. Hilo linapaswa kuwa ni jambo lenye furaha kuliko yote tujuayo." Naam.

105 "Ndipo Yeye ataonekana mara ya pili, kwa wale wote wanaopenda kuonekana Kwake," wanaopenda na kutamani jambo hilo. Ni swala la upendano. Na jinsi tunavyopaswa kupendana mmoja na mwenzake, kwa sababu sisi ni wenyeji wenza katika Mwili mmoja! Tunapaswa kuwa na upendo, mmoja kwa mwenzake.

106 Ikituonya, wakati umekaribia! Waaminio wanapaswa kuwa wakijitenga wenyewe kutoka kwa mambo ya ulimwengu, mahangaiko ya ulimwengu. Hiyo ndiyo sababu ninawakemea wanawake, na kadhalika, jinsi nilivyofanya. Halafu, basi, jitenge mwenyewe kutoka kwenye vipindi hivi vya TV! Jitenge mwenyewe kutoka kwenye uinjilisti huu wa Hollywood! Rudi kwenye undani na uaminifu! Tunasimama mimbarani, na kuruka juu-chini, na kucheka na kupaza sauti, na kufanya yasiyofaa. Wanawake wanacheza dansi sakafuni, nguo walizovaa zimewabana kwelikweli, na kila namna ya mapambo na kadhalika zinaning'inia, na nywele zilizonyolewa, na baadhi yao na vipodozi. Nao wana mchungaji wa kiakili hapo, mhubiri anayeweza kuweka neno pamoja kikamilifu kabisa. Hilo silo. Hatuji kwenye madhabahu ya Mungu, tukicheka, tukifanya yasiyofaa, na kugombana. Tunakuja madhabahuni, kwa uaminifu na kilindi, kwa sababu hapo tunakufa. Huendi, kwenye mauti, ukicheka na kuchangamka, kama una akili zako timamu. Ni mwendawazimu ndiye afanyaye hivyo.

107 Hapa majuma machache yaliyopita, nilipokuwa nikitazama ki—kipindi, kutoka kwenye moja ya vituo vya petroli nilikuwa nimesimama, cha ndugu yetu mashuhuri, Billy Graham, wakati alipokuwa akifanya uamsho wake mkubwa kuliko yote aliyokuwa nayo, au alikuwa na uamsho mkubwa zaidi huko California. Nilikuwa nikitazama hii televisheni, nilikuwa nikitazama nyuso zao wakija madhabahuni. Watoto wakipigana ngumi mmoja na mwenzake, na kupigana, wakipita kwenye madhabahu, na kucheka na kufanya mizaha, hakuna uaminifu, wakitafuna chingamu, wakiangalia kote. Wanaingia pale moja kwa moja na kusema "ndiyo," wanafanya maungamo na kurudi wakitoka. Billy alisema anaweza kuwa na elfu thelathini wa hao kwa kipindi cha mwaka mmoja, hana thelathini waliosalia. Hakuna uaminifu. Hakuna uaminifu tena.

108 Watu hawako tayari kuungama. Wanataka kuomba, "Mungu, Wewe niponye, fanya *hili*, au fanya *lile*, fanya *lile*." Lakini inapofikia kufa, na kukiri dhambi zako na kuwa sawa na Mungu, hakuonekani tena. Hiyo ndiyo sababu hatuoni tena uponyaji kuliko yale tuliyo nayo. Hiyo ndiyo sababu ninahubiri mambo haya. Hebu tuweke mambo tayari kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Lazima ufanye kitu hicho kufanya kazi kwanza.

Mungu hukuponya kwa ajili ya utukufu Wake. Nasi hatuna budi kuwa tayari kwa ajili ya utukufu Wake.

109 Sasa hilo ndilo ilibidi Misri kufanya. Kumbukeni, walichunguza mwana-kondoo kwa siku kumi na nne. Misri . . . Alisema, "Ondoeni uchafu wote kutoka nyumbani mwenu. Ondoa kila, chachu yote nje."

110 Huwezi kuwa na chachu yoyote. Wakati alama hii ikija nyumbani mwako, hii Ishara, huwezi kuwa na chachu ndani Yake. Hiyo ni ulimwengu. Huwezi kumpenda Mungu na mali, ulimwengu, kwa wakati mmoja; shughuli zote za ulimwengu, shughuli zote, na kanuni zenu za imani, na mizozo yenu, na tofauti yenu. Unamjia Yesu Kristo!

111 Ungeweza kuwazia Myahudi katika Agano la Kale, akishuka na mwana-kondoo wake, kutoa sadaka? Alikuwa anamtii Yehova, kile Yeye alichomwambia, afanye. Hiyo iliendelea. Aliikubali sadaka. Alimwona mwana-kondoo akifa. Mikono yake ilijaa damu kutokana na mwana-kondoo anayekufa. Alirudi nyumbani, amehesabiwa haki, kwa sababu alikuja kwa uaminifu. Hilo lilikuwa jema.

112 Lakini baada ya kitambo ikawa desturi. Ndipo mtu akasema, "Unajua, huu ni wakati wa pasaka, afadhali twende tufanye hili, na sina budi kutoa mwana-kondoo." Ikafikia mahali ungeweza kununua mwana-kondoo, ampate mtu mwingine kumtoa kwa niaba yake. Ikawa kanuni ya imani. Ikawa fundisho la sharti kanisani. Ndipo Mungu akasema sadaka yenyewe aliyohitaji imekuwa uvundo puani Mwake, kwa sababu ilitolewa bila uaminifu.

113 Na sisi watu wa Kipentekoste tunaingia katika hatua iyo hiyo. Hiyo ni kweli. Tumeshuka mpaka uaminifu umetoweka, miongoni mwetu. Tunaingia na kujaribu kuingiza watu kanisani, kama kanisa lingine lifanyavyo, kupata umati mkubwa, na kadhalika, katika makanisa yetu. Kamwe hatupaswi kufanya hivyo.

114 Lazima tufikie uaminifu, na hapo tufe kabisa tuwezavyo, hata Damu ya Yesu Kristo na Ishara iweze kuja juu yetu. Humfanya mtu kuwa mtu tofauti. Mwanamke anaweza kusimama kutoka hapa na aondoke, anataka kuamini kila Andiko lililo katika hiyo Biblia, haidhuru ni kitu gani kinachotendeka. Mwanamume, vivyo hivyo; hakuna dhehebu, hakuna kanuni ya imani wala chochote kingine, kiwezacho kamwe kumtenga kutoka kwenye upendo wa Mungu ambao alipata pale madhabahuni, kama ataendelea kufuata katika njia ya Bwana. Lakini leo hii hatuna uaminifu kwa hilo, tunalichukulia tu kama desturi, "Baba zetu walifanya *hili*."

115 Kama tu vile Siku ya Shukrani. Watu wengi leo hii kamwe hawakufikiria, makumi elfu mara maelfu, na mamilioni wa Marekani wanakula chakula cha kutwa leo hii katika sherehe

ya shukrani, na bata mzinga mezani, na kamwe hata hawajatoa baraka, kurudisha shukrani. Lakini wasingefanya hili bila ya kuwa nayo. Katika meza ile ile ambapo walikuwa na bata mzinga, kisaga cha wiski na bia nyingi zimewekwa kuzunguka meza. Imekuwa ni desturi.

Unasema, "Hiyo ni dhihaka. Hiyo hata si Umarekani."

116 Nitaligeuza moja kwa moja pajani mwako. Kuja madhabahuni na maungamo ya jicho kavu ni desturi. Unapaswa kufa hapo kwa Sadaka yako, unapojitambulisha mwenyewe kwamba umekufa. Amina. Umezikwa ndani ya Kristo, u—ulimwengu umekufa nyuma yako. Na inakupasa kutembea katika maisha mapya na Kristo Yesu, katika ufufuo Wake, ukilipenda Neno Lake, ukilichukua Neno Lake, mtazame Yeye akijitambulisha Mwenyewe katika Neno Lake, huku akikupa utambulisho kwamba umepita kutoka mautini kuingia uzimani. Ni wakati wa jinsi gani tunaoishi! Naam, bwana.

117 Sasa tunaona kwamba tunaishi chini katika saa za mwisho, waaminio hawana budi kukubali Neno lote.

118 Tazama, haikuwa tu kuja pamoja na kuzungumza juu yake, kwamba Wayahudi wote wanakuja pamoja na kusema, "Sasa nitawaambia nini, niwaambieni, jamani. Mnajua, ninaamini kwamba Musa yuko sahihi, kwa sababu, tazama, tunamwona Mungu akijitambulisha pamoja na Musa. Kwa sababu, tunaona ile Nguzo ya Moto, tunajua kile ambacho hutendeka. Tunajua vitambulishi vyote ambavyo Mungu amempatia Musa. Ni sahihi. Mnajua, akasema, 'Inatubidi kuwa na damu kwenye mlango.' Ninaamini hilo. Lakini, mnajua, hata hivyo, ninaamini mimi karibu ni mtu mzuri tu kama mtu mwingine yeyote. Mimi—mimi—mimi—mimi kwa kweli ni Myahudi wa agano. Nimetahiriwa na mimi hulipa sadaka zangu na zaka katika kusanyiko. Mbona, hata kuhani, mimi hula chakula cha kutwa pamoja na yeye. Vema, mimi ni mtu mzuri tu kama nyinyi wengine mlivyo." Hilo silo lililotendeka.

119 Hatupaswi kuja pamoja kuzungumza kuhusu Ujumbe. Tunakuja pamoja ili kuingia ndani ya Ujumbe. Nao Ujumbe ni Kristo, Yeye ni Neno. Hiyo ni kweli. Tunapaswa kuingia ndani Yake, tuingie chini Yake. Naam, bwana. Hilo ndilo tunalopaswa kufanya.

120 Yeye hakuwajibikia watu wowote ambao hawako chini ya damu, hata mmoja; haijalishi kwamba alikuwa ni nani, hakuwajibika. Wote iliwabidi kuchukua si yeye mwenyewe pekee, bali familia yake yote. Wako tu salama wakati i—ishara ilipowekwa hadharani.

121 Hatuwezi kujihisi salama mpaka Ishara hii iwe imewekwa hadharani. Hiyo ni kweli. Lazima uje chini ya Ishara hii, Roho Mtakatifu wa Mungu. Na Yeye humweka Yesu Kristo hadharani kwako, kwa sababu Huyo huja na kuishi ndani yako.

122 Kama nilivyosema jana usiku, na—na huko juu New York, kwenye mmoja wa Jumbe. Kama mimi—kama nilikuambia kwamba Shakespeare anaishi ndani yangu, ningefanya kazi za Shakespeare. Maana, nisingesaidia, si mimi mwenyewe tena, mimi nimekufa. Mimi na Shakespeare hatuwezi kuishi pamoja hapa ndani. Shakespeare alikuwa mshairi, na mimi ni mhudumu, hatuwezi kuishi pamoja. Lakini kama nimekufa kwa nafsi yangu, basi, naye Shakespeare anaishi ndani yangu, kazi za Shakespeare nitazifanya. Maisha ya Shakespeare ndani yangu yataishiwa kama Shakespeare. Kama uhai wa Beethoven ulikaa ndani yangu, ningekuwa Beethoven. Kama uhai wa John Dillinger ulikaa ndani yangu, ningekuwa John Dillinger. Hiyo ni kweli.

123 Na kama Uhai wa Yesu Kristo unakaa ndani ya mtu, wanatambulishwa na Yeye. Ni Kristo ndani yako. Si mshiriki wa kanisa, si mfumo, bali Nguvu zilizofufuka. Ni Roho Mtakatifu, ni Ishara juu yako, hata maisha yako yanasema "amina" kwa kila Andiko. Ahadi imeandikwa humo ndani.

124 Na wewe si wewe mwenyewe tena. Wewe ni wa Kristo. Huwazii mawazo yako. Huwazii mawazo yako, unasema, "Nafikiri." Huna wazo lolote lijalo. Ule Uhai uliokuwa ndani ya Kristo umo ndani yako. Nia iliyokuwa ndani ya Kristo imo ndani yako. Kazi zilizokuwa ndani ya Kristo zimo ndani yako, na Kristo Mwenyewe yumo ndani yako. Wewe umekufa; maisha yako yamefichwa ndani ya Mungu kwa njia ya Kristo, yakatiwa muhuri humo ndani kwa Roho Mtakatifu. Wewe si wako mwenyewe.

125 Yeye hakuwajibika kwa mtu yeyote. Familia nzima lazima iletwe ndani, na ishara lazima iwekwe hadharani. Ilibidi iwe hivyo. Kama haikuwekwa hadharani, basi haikufaa kitu. Ungeweza kuiamini, ungeweza kusema, "Loo, naam, ninaiamini." Lakini hiyo haikuitimiza. Hiyo, unasema, "Vema, nitakuambia nitakachofanya. Nitaiweka katika ndoo, kisha nitaiweka hapa kwenye ukuta. Lakini kwa kweli, nafikiri, mradi tu mimi—mradi ninayo humu ndani, kama nilikuwa na damu *hapa*." La, bwana.

126 Huwezi kuwa mvulana wa siri kuhusu Hiyo. La, bwana. Inakubidi kuwa na Hiyo! Inakubidi kuiweka Hiyo hadharani. Hilo lilikuwa ndilo kusudi la kuiweka kwenye milango, ili Yeye aweze kuiona kwenye kizingiti na kwenye mwimo wa mlango. Ni kitu ambacho hukionei aibu. Unataka ulimwengu wote ujue kwamba umekufa, na maisha yako yamefichwa ndani ya Mungu kwa njia ya Kristo.

127 Zungumza kuhusu Siku ya Shukrani, nakwambia, si desturi, hata kidogo. Tunazo desturi nyingi sana sasa. Tunachohitaji leo hii ni kufanywa upya, ubatizo wa Roho Mtakatifu kurudi kanisani; si sherehe, bali kujazwa. Basi hiyo inapaswa kuwa

ndiyo sherehe yetu ya Siku ya Shukrani, vile tungeiita. Inapaswa kuwa ni Roho Mtakatifu akija katika maisha yetu. Kama tungeweza kula bata mzinga kama babu zetu walivyokula, tunapaswa kumpokea Roho Mtakatifu kama babu zetu walivyokuwa naye. Amina. Si desturi, bali amri kutoka kwa Mungu. Tunapaswa kumpokea Huyo.

128 Mwangalie Yoshua, na usome Yoshua, mlango wa pili. Nimeandika hapa chini, "Isome Hiyo." Sina wakati. Bali ninawatakeni mjue, wakati Musa na Yoshua walipokuwa njiani kupitia nyikani, wakija kwenye kutoka, walituma baadhi ya wahudumu, wapelelezi, kwenda kuipeleleza nchi. Pia kumbuka, kulikuwa na Mtaifa huko ng'ambo ya pili ya mto, jina lake Rahabu. Alikuwa kahaba. Maskini mtoto huyo alikuwa mzurura mtaani, labda aliyefukuzwa na familia yake. Lakini tunaona ya kwamba wakati alipowaona wale watu na kujua kwamba walikuwa ni watu wa Mungu, yeye alikuwa ni kahaba, na alitaka kujua kama kungeweza kuwapo na rehema yoyote angaliweza kujaliwa.

129 Mungu huwapa rehema wale wanaoitia rehema. Wote wanaoitia rehema watapokea rehema.

130 Mtazame huyu kahaba, alisema, "Nitaonyesha fadhili." Tazama, haikumlazimu kumwona Yoshua. Hakujua jinsi alivyochana nywele zake, nguo alizovaa. Alisema, "Nimesikia kwamba Mungu yu pamoja nanyi." Hayo tu ndiyo aliyotaka kujua.

131 Nami ninakuambia, leo hii, ndugu, si jinsi unavyochana nywele zako, ama kile ufanyacho, ama aina ya nguo unazovaa, aina ya Ph.D. uliyo nayo. "Ninasikia kwamba Mungu yuko miongoni mwenu," hilo ndilo jambo kuu. Tunataka kujua mahali Mungu alipo miongoni mwa hili.

132 Yatazame madhehebu. Tazama mahali yanakoenda. Je! Mungu yuko miongoni mwa madhehebu? Kama ni hivyo, basi Yeye anawaongoza moja kwa moja kuelekea Baraza la Makanisa, na kurudi kwenye alama ya mnyama. Mungu hayuko katika hilo.

133 Mungu yuko katika Neno Lake, kwani Yeye ni Neno. Hiyo ni hakika. "Nimesikia." Nayo imani huja si kwa kusikia baraza, bali Neno. Kusikia Neno!

134 Waliona hili, nao wakajua. Alijua ilikuwa ni kweli. Aliomba rehema, tazama, kwa ajili yake na familia yake pia. Aliomba kwa ajili yake na familia yake, kama vile tu walivyofanya huko Misri.

135 Tazama, alipewa ishara, ishara nyekundu. Kwamba ile kamba nyekundu ambayo aliwateremshia wale watu, wapelelezi, chini kupitia dirishani, ingekuwa ni ishara. Mungu asingeninii, malaika wa kuangamiza . . . Malaika wa Mungu wa kuangamiza asingekuja karibu na yeye mradi tu alikuwa na hiyo ishara. Bali, na vipi kama angaliweza kusema, "Loo, niliwateremsha. Nilifanya—nilifanya tendo jema. Kwa hiyo sasa ili kuzuia mtu

yeyote asinikosoe, na kuona kamba hii nyekundu ikining'inia hapa nje, nitairudisha kamba hiyo juu"? Ndipo ninii . . . malaika wa hukumu asingalipita juu ya nyumba yake. Ilimbidi awe na ishara imewekwa hadharani. Ilibidi ibakie pale.

136 Haleluya! Loo, inamaanisha, "msifu Mungu wetu," katika majira haya. Kumbukeni hili. Sipo hapa ndani kwa ajili ya riziki. Sipo hapa ndani nikihubiri ili kupata riziki. La, bwana. Ninaweza kuifanyia hiyo kazi, hata hivyo. Sifanyi hii kwa ajili ya hiyo. Kama niliwazia kwamba kulikuwako na njia yoyote nyingine kando na hii sahihi . . . Kumbukeni, huyu ni mimi, inanibidi kukutana na Mungu. Ni nafsi yangu. Inabidi iwe ni mimi. Sio tu mimi, lakini ningekuwa na hukumu zaidi. Neno la Mungu ni Mungu. Huo ni mpango wa Mungu uliowekwa hapo, na hiyo ni Kweli.

137 Ninaamini kwamba utepe huo mwekundu ilibidi uwekwe hadharani, au malaika, malaika wa kuangamiza, asingaliheshimu chochote kingine ila ishara hiyo wakati iliwekwa hadharani. Wajumbe walimpatia ishara, na yeye lazima aidumishe imewekwa hadharani.

138 Tazama, Yeriko ilikuwa imesikia kile Mungu alikuwa amefanya, lakini haikufanya chochote ili kuchukua onyo hilo.

139 Ulimwengu leo hii, haujafungiwa pembeni mahali fulani, ulimwengu mzima unajua mambo haya yanaendelea. Ulimwengu wote umejua. Waespikopolia, Katoliki, Lutheri, madhehebu yote wanajua kwamba kuna Mungu ambaye hufanya kazi katika Neno Lake katika siku hii, na hufanya ishara Zake na maajabu kuendelea. Hazijafungiwa mahali fulani kwenye kona. Walisikia Hilo, bali hawakutaka kupokea Hilo. Walikuwa wamelisikia.

140 Nguvu Zake kuu na ishara Zake zilikuwa zimewekwa, kuonyeshwa hadharani, lakini hawakutaka kupokea Hilo. Sawa tu na vile ilivyokuwa huko Sodoma, ishara Zake kuu na maajabu zilikuwa zimeonyeshwa kule, bali hawakutaka kupokea Hilo. Kwa hiyo hakukuwa na chochote kilichosalia ila hukumu, ilikuwa inafuata. Hawana budi kuamini Neno lote, ili kuwa salama. Lakini wao walifikiria kwamba walikuwa salama, labda, katika dhehebu lao kubwa la Yeriko, mji wao. Walidhania hilo lilikuwa zuri vya kutosha, lakini halikuwa hivyo.

141 Lakini maskini kahaba mmoja. Hapana budi kulikuwako na wavulana fulani wa kanda waliojipenyeza mle ndani na kucheza baadhi ya kanda. Mbe—mbegu iliyochaguliwa kimbele ililishika na kuliamini. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, waliingia kule kwa ajili ya ujumbe. Walikuwa na kanisa usiku huo katika nyumba yake. Alitumia nyumba yake kama kanisa, kupokea ujumbe.

142 Ee Mungu, jalia tufungue mioyo yetu na kupokea Ujumbe, kwamba Yesu yu hai usiku wa leo. Yupo papa hapa miongoni mwetu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ifungue

nyumba yako na umruhusu Mjumbe, Roho Mtakatifu, aingie na kukutambulisha kwa Uwepo Wake Mwenyewe, Ishara iliyoko juu yako. Ndipo huna haja ya kuchukua neno la mtu yeyote mwingine kwa hilo, Yeye yupo kujitetea Mwenyewe. Na Yeye ni Neno. Hiyo ni kweli. Ni Ishara ya Mungu, kujitambulisha Yeye Mwenyewe.

143 Alitumia nyumba yake kwa ajili ya wajumbe. Ndipo akaingiza mji wote, ulioweza kuamini, chini ya ishara iyo hiyo.

144 Na hivyo ndivyo kanisa linavyopaswa kuwa likifanya leo hii, kuingiza kila kitu kitakachoamini, chini ya Ishara. Ishara ni Roho Mtakatifu. Kumbukeni tu, hawana budi kuingia chini ya Roho Mtakatifu.

145 Basi wakati Mungu alipokuwa amewaangamiza malaika wake. . .Malaika wa kuangamiza alipitia, ndipo wakati walipoiona ile alama ya ishara, nyumba yake ilisimama. Yeriko wote uliporomoka. Lakini kupigwa tu kwa baragumu, hebu wazia tu, na kuta zote zikaanguka. Walienda moja kwa moja na kuua kabisa kila kitu kilichokuwemo humo, lakini wote waliokuwa chini ya ishara hiyo walikuwa salama. Kwa nini? Mjumbe wa Mungu alikuwa amekuja. Walikuwa wamewaambia ukweli na wakaingia chini ya ishara. Naam bwana. Ila wengi wao hawakutaka kuamini hilo. Kwa hiyo kama hawakutaka kuliamini, iliwabidi kukabiliana na hali.

146 Uhai ule ule uliokuwa ndani ya ishara kule Misri, unaona, uhai, kitu kile kile kama ishara ya uhai huko Misri.

147 Walipoteremsha ile kamba chini, hiyo ilikuwa ndiyo ishara. Katika ulimwengu huo wa Mataifa, hakukuwa na damu iliyowekwa kwa ajili yao bado, lakini walitoa alama ya wekundu, ya ishara. Kwa hiyo, walipoiona ishara; Yoshua, mfano wa Yesu, alikuwa mwaminifu kwa ishara na alama ambayo wajumbe wake walikuwa wamehubiri, wakati Yoshua alipotoa amri kwamba mtu yeyote asiende juu kwenye ile nyumba ambapo hiyo ishara ilikuwapo (la, bwana), kwa sababu hakuna mtu aliyepaswa kuuawa chini ya ishara hiyo. Na *Yoshua* hakika linamaanisha "Yehova Mwokozi," sawa na vile Yesu linavyomaanisha. Basi wakati alipotuma wajumbe wake, Yoshua, mfano mwingine kwa ulimwengu wa Mataifa, na Mataifa, lile kundi dogo lililoamini na kuweka ishara hii hadharani, hata malaika wa kuangamiza aliitambua ishara hiyo. Unaona?

Hilo ndilo jambo pekee ambalo Yeye atatambua leo hii.

148 Kamwe hakutambua rais wa kundi hilo. La. Hakumtambua mtu mkuu, majemedari wa vita, mtu mashuhuri. Yeye kamwe hakuwatambua. Yeye alitambua tu mahali ishara iliwekwa hadharani. Wengi wao huenda waliliamini. Wengi wao huenda waliamini kwamba walikuwa wanaenda kuchukuliwa, lakini hiyo haikulizuia. Ishara ilibidi iwekwe hadharani. Naam,

bwana. Hayo tu. Wote chini yake waliokolewa, huko Misri. Na wakati huo huo, wote chini yake waliokolewa huko Yeriko.

149 Mwana-kondoo aliyejawa damu ndiye Ishara yetu usiku wa leo. Katika Waebrania 13:10 na 20, inaitwa "agano la milele," kama ungependa kuisoma. Ahadi za Mungu zenye msingi katika damu zilituweka huru na dhambi na mwili. Ni agano la milele, kumwabudu Yeye na kuonyesha ishara Zake zilizoahidiwa. Agano Jipya ni mkataba mpya katika Damu Yake. Biblia ilisema hivyo. *Agano Jipya* maana yake ni "mkataba mpya," Uhai wa Damu, Uhai mpya wa Ishara ndani yetu. Mahali ambapo damu ya kale ilisimamia ishara rahisi ya kemia kwamba mwana-kondoo alikuwa amekufa, Roho Mtakatifu ndiye Uhai uliokuwamo ndani ya Utu wa Yesu Kristo uliodhihirishwa ndani yako na mimi, usiku wa leo. Nje ya hiyo, hakuna rehema. "Ni wakati tu nitakapoona damu, nitapita juu yako."

150 Ninajaribu kukazia katika nia zenu, rafiki, kwamba wakati umewadia, ambapo jambo fulani halina budi kufanywa na hiyo. Lazima tufanye jambo. Ama iko ndani au nje. Hayo tu. Saa imewadia ambapo Ishara lazima iwepo. Ikiwa hii kamwe. . . Ikiwa kanisa hili kamwe linatarajia kubakia hai mpaka Yesu Kristo atakapokuja, Ishara itabidi iwe hapa. Hivyo tu. Kifo kisipofanya, itachukua alama ya kifo. Na karibuni, iko katika mjadala sasa hivi, mashine kubwa imeandaliwa kufanya makanisa yote kuingia katika muungano huo wa makanisa.

151 Na wewe afadhali kweli uwe na Ishara ikiangaza. Lakini wakati umewadia kwa ajili ya kutoka. Basi wakati huu tunaenda katika Nchi ya ahadi, ahadi ya Uzima wa Milele. Ishara hii inaonyesha kwamba Yesu Kristo . . . Roho Mtakatifu anaonyesha kwamba Yesu ametimiza kila hitaji kwa ajili yetu, kwamba sisi, katika asili yetu, ni wana wa Mungu walioanguka. Na sisi hatuna nguvu ndani yetu. Hatuna Uzima ndani yetu. Sisi ni jamii ya watu walioanguka, kuanzia Adamu. Lakini wakati tunapoweza kuonyesha hiyo Ishara, kwamba Neno na sisi tunakuwa kitu kile kile, inaonyesha kwamba Yesu Kristo alitimiza hitaji kwa ajili ya dhambi yetu na mauti, na ameonyesha Ishara Yake ndani yetu. Loo, jinsi inavyoweza kuwa rahisi! Umehukumiwa. Sisi sote tulihukumiwa. Hakuna njia ya kujiokoa wenyewe, ndipo Mungu akatutumia Ishara. Alimwua Mwana Wake pale Kalvari, kwa ajili yetu. Nao Uhai uliokuwa katika hiyo Damu, wakati Hiyo ilipomwagwa pale Kalvari, umerudi kuwa Ishara juu yetu.

152 Ishara ya Mungu ya Milele, isiyo na mwisho, Hiyo ni Uzima wa Milele kwa Mungu wa Milele. Na chochote kilichokuwa na mwanzo kina mwisho, na kila kitu kilikuwa na mwanzo mbali na Mungu. Na Mungu ndiye aina pekee ya Uzima wa Milele iliyopo. Basi wakati Mungu akitia Roho Wake Mtakatifu ndani yako, ambaye ni Mungu, na wakati Mungu akijitia Mwenyewe ndani yako, wewe ni wa Milele kama Mungu alivyo. Kwa sababu, wewe ni sehemu Yake, kwa sababu unafanyika mwana au binti

wa Mungu na unaonyesha Neno Lake. Haleluya! Ninajihisi wa kidini. Hiyo ni kweli. Mungu huitambulisha, Mwenyewe. Uko na Uzima wa Milele, na huo ni Mungu ndani yako. Nalo Neno hili ni Mungu. Na hilo Neno huishi na kujizaa Lenyewe. Kile tu hasa ambacho Mungu amekusudia kwa ajili ya wakati huu, unacho, amina, Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu akidhihirishwa. Naam, bwana. Ni kitu gani? Roho Mtakatifu, Neno limehuishwa kwako na Roho Mtakatifu, kuthibitisha wakati huu, kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

153 Na sasa wewe ni Wake. Loo, kwa sababu Yeye yupo, tunayo haki kwa yote ambayo Yeye ametununulia. Kila ahadi katika Biblia ni yako. Ni mali yako, wakati Ishara hii ikiwa juu yako na Mungu amekutia muhuri. Sasa tunataka kujichunguza wenyewe kwa muda mfupi tu. Wakati Mungu amekupatia ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu, basi Uzima wa Yesu Kristo umo ndani yako. Sasa, hiyo ni kweli, na kila mwanatheolojia itabidi akubali hiyo kuwa ni hivyo. Naam, bwana. Ni Kuzaliwa kupya. Unazaliwa upya, kwa Roho Mtakatifu. Na kwa sababu Mungu ametenda hili, na unajua kwamba wewe si mwema kwa nafsi yako, na unakubali kile Mungu alichofanya, basi Yeye anakutia muhuri katika Ufalme Wake, kwa Roho Mtakatifu. Ndipo kila kitu ambacho Yesu alinunua na kukuahidi, katika Biblia, ni chako. Ni mali yako kwa sababu imelipiwa. Amina. Uzima ni wangu; Yeye alilipia Huo. Uzima ni wako; Yeye alilipia Huo. Uponyaji ni wangu; Yeye aliulipia. Uponyaji ni wako; Yeye aliulipia. Uhuru ni wangu; Yeye aliulipia. Mbingu ni yangu; Yeye aliilipia. Ameishalipa gharama. Kila kitu ambacho Yeye alinunua ni mali yake yule aliye na Ishara. Amina. "Kupita Ishara Yangu," juu ya motokaa ya mtaani, "kwenye Siku hiyo ya Hukumu, nami nitapita juu yako." Amina. Kushikilia Hiyo ndani! Kushikilia maungamo yako katika Neno, kwamba Yesu Kristo amekufa kwa ajili yako. Basi wakati akifanya hivyo, Yeye hujionyesha Mwenyewe wazi kupitia wewe. Amina. Naam. Ukitambua Ishara, Uhai uliohitajika kwa Damu kuweza kunena!

154 Utasema, "Damu inanena? Ngoja kidogo, Ndugu Branham!" Damu hunena. Biblia inasema hunena. Vema.

155 Damu hunena. Kumbuka, Damu ya agano haitambuliwi pasipo Ishara. Sasa Neno linatuhakikishia ile ahadi. Ishara ndiyo thibitisho kwamba ununuzi umefanywa kwa ajili yetu, na Mungu ameikubali.

156 Unapoenda na kusema, "Ninataka ku—kusafiri hadi Mjini New York." Wanafanya nini? Wanakupatia tikiti. Ni kitu gani? Ni ishara. Sio fedha. Ni ishara, lakini inahitaji fedha kuinunua.

157 Sasa, unapotaka Uzima wa Milele, unapokea Ishara, inayoonyesha kwamba gharama imelipwa. Si Damu, bali ni Ishara ya Damu. Ni Uhai Wenyewe. Amina. Utiifu mkamilifu

kwa Neno lote la Mungu, kwa Neno lote la Mungu, utakupa haki kwa hii Ishara.

158 Unafanyaje hilo? Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, ile Ishara. Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu."

159 Wakati walipoona onyesho hilo la ajabu la Nguvu za ufufuo, yeye (Petro) alisimama pale na kunukuu Maandiko ya Yoeli, na kadhalika, akatoa ahadi kwa ajili ya wakati huo, na kuonyesha matakwa ya wakati huo yalikuwa yametimizwa ndani ya Yesu Kristo, na kwamba Yeye alikuwa ameituma Ishara ya Kifo Chake kurudi. Nayo Ishara hiyo ilikuwa juu yao. Ndipo akasema, "Ishara ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu, itawabidi kuwa na Ishara hii." Amina. Si kwamba wao "huenda ikawapasa" kuwa na Hiyo. "Watakuwa na Hiyo! Mtapokea Roho Mtakatifu."

160 Wakati ukilitii kikamilifu Neno la Mungu, katika—katika kujisalimisha kukamilifu kwa Hilo, wewe una haki kwa Ishara. Naam, bwana. Utiifu! "Si yeye asemaye, 'Bwana, Bwana,' bali yeye atendaye mapenzi." Basi tunapoomba, lazima tuwe na Ishara kuwasilisha pamoja na maombi yetu.

161 Hasa tu kama tufanyavyo wakati tukienda kwenye—tukienda kwenye kituo cha mabasi, tuseme, "Ninataka kusafiri."

"Unaenda wapi?"

"*Fulani-fulani*!"

162 Inakubidi kuwa na ishara, kama ishara inahitajika. Lazima uwe na ishara. Unasema, "Vema, ngoja kidogo, mimi—mimi ni Bw. Jones! Sasa hebu. . . " Hiyo haileti tofauti yoyote, lazima uwe na ishara. "Vema, nikwambie nini, ni—ninaharakisha kwenda kazini mwangu. Sina wakati wa kucheza." Ama utakuwa na ishara au hutakuwa na ishara. Ikiwa huna ishara, hutasafiri.

163 Kama una tikiti na uende hapa nje kwenye ndege, na kusema, "Ninataka kwenda Mjini New York."

"Tikiti? Ishara?"

164 Unasema, "Vema, ni—ni—nitakuambia, sina. Mimi ni jamaa mzuri sana. Nitakulipa siku moja." La, bwana, wewe kuwa na ishara, inakubidi kuwa nayo mkononi mwako. Lazima iwekwe wazi. Lazima. Loo!

165 Unaona ninachomaanisha? Lazima uwe na Hiyo! Hupaswi tu kufikiria hivyo; lazima iwe Ishara iliyotambulishwa. Kweli. Hiyo

inakupa haki, wakati ukilipa. . .wakati unapokubali gharama ambayo imelipwa. Naam, bwana.

166 Paulo anatuambia, akinena kuhusu kuzungumza kwa damu, Paulo anatwambia kwamba damu huzungumza. Mnaamini damu huzungumza? Katika Mwanzo 4:1, ama 4:10, Mungu alimwambia Kaini, Yeye alisema, "Yu wapi ndugu yako?" Akasema, "Damu yake, sa—sauti yake. . .Damu ya ninii yake, sauti ya damu yake inalia dhidi yako."

167 Sasa tunaona pia katika Waebrania, mlango wa 12 na kifungu cha 24, kwamba Agano Jipya, Damu hunena mambo yaliyo bora. Damu inanena. Basi Damu inayo Sauti. Nayo Sauti ya Damu ni Neno. Haleluya. Hiyo ndiyo inayofanya iwe ni sahihi au si sahihi. Ne—Neno linatambulishwa na Sauti ya Damu. Sauti ya Damu ni Roho Mtakatifu. Huyo huleta Uzima. Ni Uzima, na Huyo huleta Uzima kwenye Neno na kulihuisha Hilo. Amina, amina, amina.

168 Hakika, Damu hunena, Hiyo hunena kitu bora. Agano la Kale, damu ilizungumza kuhusu hatia. Katika Agano Jipya, Hiyo hunena kuhusu ukombozi. Katika Agano la Kale, ilinena kuhusu kifo na huzuni. Katika Agano Jipya, Hiyo hunena kuhusu ufufuo na Uzima. Inazungumza kuhusu uponyaji. Inazungumza kuhusu furaha. Inazungumza kuhusu Nguvu. Inazungumza kuhusu Uzima. Inazungumza kuhusu Mbingu. Na Damu iyo hiyo iliyomwagwa juu ya nchi, iliyolilia ndugu yake aliyefariki, au iliyolia dhidi ya ndugu yake aliyemwua. Damu ya Yesu Kristo hufunika dhambi zetu zote, na hunena amani na ufufuo, na Nguvu na Uzima, na uponyaji. Na baraka zote za ukombozi ambazo Damu ilimwagwa kwa ajili yake, Hiyo hunena kwa ajili yetu. Hakika, Damu hunena. Loo, jamani!

169 Lazima tuamini kwa ajili yetu wenyewe, kama walivyofanya huko chini Misri, na pia kwa ajili ya nyumba; kama walivyofanya Misri na Yeriko, na kadhalika. Pia tunakuta kwamba, nina Andiko nililoandika hapa, linaloitwa Matendo 16:31, ambapo kwamba akida wa Kirumi alikuwa aondoe uhai wake mwenyewe, na alikuwa anaenda kujichoma kisu hata kufa, ndipo Paulo akamwambia "Mwamini Bwana Yesu Kristo, na yako na nyumba yako mtaokolewa." Haina budi kuwa ni nyumba. Ni kitu gani kilichofanya watoto wengi wadogo. . .Ni kitu gani ambacho huwafanya wanawake wengi kuwa mtaani? Ni kitu gani kinacholeta upotovu mwingi wa watoto? Kwa sababu hatuwezi kuweka nyumba yetu chini ya Damu.

170 Watu wengine walisema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa. Mama alienda huko juu, na ni—ni—ni—niliwekwa wakfu huko, kama mtoto mchanga."

171 Lazima uiweke hadharani Ishara. Naam, bwana. Ondoa takataka zote za ulimwengu, mambo yote ya ulimwengu, maana huwezi kuyapenda mambo ya ulimwengu, kutokuamini kwako

kwote katika Neno la Mungu. Kumbuka, Yeye aliahidi mambo haya katika siku za mwisho. Chochote katika maisha yako, ambacho-ambacho ni kinyume na Hilo, kitoe nje, na uwe tayari na kuleta Ishara ndani. Ndipo uweke Ishara kazini, katika maombi, na kujiweka wakfu, na ushawishike na kuhusika juu yake.

172 Ikiwa tungeweza kusoma hapa, Waefeso 2:12, lingekuwa la kushtusha kwetu. Tazama, "mtumikie Mungu aliye hai," pamoja na ishara zilizo hai, amri zilizo hai. Waebrania 9:11 — 14, inatwambia vivyo hivyo. Na sisi—sisi hatutumikii makala iliyokufa (hatutumikii) au amri. Tunamtumikia Mungu aliye hai, pamoja na ishara zilizo hai.

173 Sio, "Mimi huenda kanisani. Nilijiunga. Ninaijua kanuni ya imani. Ni—ninaijua katekismo." Hizo ni desturi zilizokufa.

174 Lakini Ishara ya kweli ya Damu, ikinena, hunena kuhusu Uwepo ulio hai, uliofufuka, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele; kweli, anayeishi hivi sasa miongoni mwetu. Amina. "Inanena vema zaidi." Kutoka si kwa desturi zilizokufa na kanuni za imani, bali Ishara iliyo hai ya Kristo aliye hai aliyefufuka ambaye anaishi ndani yetu. La, wanakana kwamba kuna kitu kama hicho, bali sisi tunajua Hilo ni kweli. Lakini sisi tunaoamini Neno, tunajua kwamba Mungu aliahidi Hilo na Yeye hutimiza ahadi Yake, tunajua ni Uwepo Wake ulio hai, kwa kuwa Yeye hufanya kama Yeye alivyofanya.

175 Ikiwa ndani yako, na wewe unasema, "Vema, mimi siibi. Sisemi uongo." Vema, hicho ni kitu tu unachoweza kuacha. Unaweza kuacha kuiba, uache kusema uongo, mtu mwema mwadilifu hufanya hivyo. "Mimi hutimiza Amri Kumi." Walifanya hayo kabla Yesu hajafa. Naam.

176 Lakini, jambo ni kwamba, Kristo anaishi ndani yako! Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," ikithibitisha ya kwamba Mungu amemfufua kwa ajili yetu, kutoka katika wafu, kulingana na Neno Lake lililoahidiwa. Ni utambulisho kwamba Yesu Kristo anaishi usiku wa leo. Tunakubali damu Yake iliyotolewa sadaka, kwamba Yeye alitoa uhai Wake. Muhuri wa Ishara, ya Roho Mtakatifu, ndiyo ahadi yetu. Waefeso 4:30, ilisema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu."

177 Tukibatizwa kwa Ishara hii, katika Mwili wa Kristo, Wakorintho wa Kwanza 12, sasa sisi tuko chini ya karama za Roho zilizoko mle ndani. Ulimwengu hauamini karama. Kanisa haliamini karama. Bali Neno la Mungu linasema kuna karama. Na inachukua tu Ishara hiyo kutambulisha karama hizo. Hakika.

178 Na ndani Yake umo utimilifu wote. Ndani Yake umo utimilifu wote wa Mungu, utimilifu wote wa ahadi. Tukibatizwa

ndani Yake, tunayo kila ahadi, ambayo Mungu aliifanya, imewekwa katika ncha za vidole vyetu. Hamna dhambi mle. Hamna mauti mle. Na hata ugonjwa hauwezi kukaa katika Uwepo Wake. Shetani basi akiweka mikono yake kwako na kujaribu kukujaribu kuingia katika kitu fulani, wewe shikilia Ishara yako mikononi mwako na uionyeshe, kwamba wewe ni bidhaa iliyokombolewa ya Yesu Kristo. Amina. Acha imani yako isiyoghoshiwa itikise Ishara hiyo hapo, na kusema, "Mimi ni bidhaa ambayo Yesu Kristo alinunua." Amina. Ugonjwa unatoroka!

179 Ni kitu gani kilichokifanya kile kivimbe kikubwa kutoweka ndani ya mke wangu hapo jana? Wakati siku chache tu zilizopita, alikuwa tayari kwa meza ya upasuaji, na sasa hawawezi kupata kitu. Ni kwa sababu nguvu za kufufuka za Yesu Kristo, ile Ishara ya Mungu, kwamba Yeye angali anaishi. Hiyo ilikiangamiza.

180 Ni kwa nini mambo haya hutendeka? Ni kwa sababu Mungu aliahidi. Wewe ni bidhaa. Shikilia Ishara, katika imani yako isiyotikisika katika Neno Lake la ahadi. Mungu mara moja alitupatia Ishara . . .

181 Ninapofunga, sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi. Tutaondoka kufikia saa tatu u nusu.

182 Mungu aliupa ulimwengu ishara, wakati mmoja, ilikuwa ni upinde wa mvua. Aliwapa ishara, kwamba Yeye kamwe asingeangamiza ulimwengu kwa maji tena. Na Yeye daima amedumu mkweli kwa ishara hiyo. Amina. Hajakosa kuiweka hadharani. Mungu alifanya ishara, kasema, "Nitawapa ishara. Na wakati nikiwaahidi hii, kila wakati mvua inapokuja, nitawaonyesheni ishara hii." Basi Mungu, wakati Yeye anapofanya ishara, Yeye huonyesha Yake, maana hayo ndiyo Yeye aliyoahidi kufanya. Na Yeye anatutarajia kufanya jambo lilo hilo. Yeye daima alibaki mwaminifu kwa ishara Yake.

183 Na ikiwa tumezaliwa kwa Roho wa Mungu, daima tunabaki waaminifu Kwake. Kama wewe ni namna fulani ya kitu cha kuchochewa kwa njia ya kubuni, ulikuwa na namna fulani ya msisimko, ukajiunga na kanisa fulani, ukafanya namna fulani ya mhemko, labda ulinena kwa lugha, ama ulipaza sauti, ama uliruka juu chini, ama uliimba katika Roho, kama mnavyokuita. Nimeona mambo hayo yote yakionyeshwa miongoni mwa makafiri, unaona. Hiyo haimaanishi chochote. Lakini wakati kwa kweli bidhaa, Uhai mpya wa Yesu Kristo, unakuja ndani ya mwanamume au mwanamke, yeye ni kiumbe kipya, mtu wa kale amefariki. Amekwisha. Amekwisha. Ishara hiyo lazima iwekwe wazi daima.

184 Mungu alionyesha Yake. Tazama, maelfu haya yote ya miaka, Yeye hajawahi kushindwa kuiweka hadharani kwetu. Yeye ni mtiifu na mwaminifu kwa ishara Yake, akituonyesha kwamba Yeye kamwe hakosi kuheshimu Kile Yeye amefanya.

Kamwe hakosi kuheshimu! Tunaona upinde wa mvua, na huo unaonyesha kwamba Mungu alitupatia ahadi hiyo. Na Yeye alisema itakuwa hivyo, na Yeye kamwe hakosi kuliheshimu Neno Lake. Yeye daima ataliheshimu Neno Lake. Huthibitisha hivyo, katika hilo. Kila ishara aliyotoa, Yeye hudumisha Neno Lake.

185 Loo, Mungu, Yeye alituahidi Ishara. "Basi nitakapoona damu, nitapita juu yenu. Nayo damu itakuwa ishara kwenu."

186 Loo, mwenye dhambi, usiku wa leo, unawezaje kuondoka mahali hapa, kutoka chini ya hiyo Ishara? Unawezaje kubahatisha juu ya ufuasi wa kanisa lolote au chochote kingine? Unawezaje kumudu kufanya hivyo, ukiona tunaishi katika wakati ambapo hamna matumaini katika siasa, hamna matumaini katika siku za usoni? Kitu pekee kilichoko ni Kuja kwa Yesu Kristo, Kuja kwa Kristo kuchukua Kanisa Lake.

187 Ungewezaje kwa akili timamu kuondoka kutoka orofa hii ya chini, uondoke kutoka katika chumba hiki, au mahali pengine, na kujiaminisha mwenyewe katika kanuni fulani ya imani ama kitu fulani ambacho umekuwa ukinukuu, ambacho hakionyeshi alama yoyote ya Ishara ya Uzima na Yesu Kristo wa kawaida, na—na kuja na kuzalisha yeye yule jana, leo, na hata milele, na kudhihirisha Neno Lake kama Yeye alivyoahidi kufanya; na halafu ungeweza kusimama na kusema, "Siku za miujiza zimepita," ukiwa na Ishara yenyewe ya Mungu Mwenyewe ndani ya maisha yako?

188 Mungu anaonyesha Ishara Yake sasa. Na Yeye daima atakuwa mwaminifu kwa Hiyo. Katika saa ya kifo chako, Malaika wa Mungu watakuja na kukubeba kutoka katika mauti, na kabla hukumu kuu kuupiga ulimwengu.

189 Tena tunasoma huko katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu." Sasa, tafsiri ya kweli ya hilo si "yeye asikiaye." Hiyo ni ya Mfalme James. Tafsiri halisi, katika Kiebrania katika hilo, ni hii, "Yeye *alipokeaye* Neno Langu." Si yeye alisikiaye; yeyote anaweza kusikia Hilo, wenye dhambi na kila kitu kingine. Bali, "yeye alipokeaye," anayeweza kuchukua Hilo lote. Si, "yeye alipokeaye *moja* ya Maneno Yangu." "Yeye alipokeaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka." Unapolipokea Neno, unampokea Yeye. Kila kitu Yeye alichosema ufanye, kwamba wewe uko tayari na unafurahia kufanya. "Yeye apokeaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, ana Uzima wa Milele, wala hatapitia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Loo, ni ahadi ya jinsi gani! "Nionapo Ishara hii, nitapita juu yenu."

190 Yeye anatutarajia sasa kuonyesha Ishara Yake kwa makundi yote yasiyoamini ya Shetani na madhehebu ya ulimwengu huu, kwamba tunaamini kwamba kile ambacho Yeye ameahidi (kama uzao wa Ibrahimu) Yeye ana uwezo wa kutimiza. Haijalishi jinsi ilivyo ya kisayansi, ni wanaanga wangapi, wanasayansi

wangapi, wanasimama na kuthibitisha *hili* au kuthibitisha *lile*, na mwaka ujao inawabidi kulighairi, hatujali wanachosema. Elimu yetu yote kamwe haiwezi ikakupa Uzima.

191 Ninaishi katika jiji ambapo Chuo Kikuu cha Arizona kimo. Na ninaona nini huko ila uchafu na uozo, na shule za sekondari za juu na mambo ya jiji hilo; hivi majuzi, walikuwa na wavulana na wasichana matineja mia nne wakiwa wamevua nguo zao, na vipipa vya pombe, wakicheza dansi katika mahali pakubwa juu huko Sabino Canyon huko juu. Watoto hawa wote wadogo wanatoka nyumbani, na kadhalika, hapo karibu, unawakuta huko juu, kutoka chuo kikuu. Tuna kitu gani? Chuo kikuu kinaweza kukuambia kile kilichotumiwa kutengeneza mbegu, bali hakiwezi kuipa mbegu uhai. Elimu yako hukupeleka tu mbali na Mungu.

192 Yupo Mmoja tu awezaye kukupa Uzima. Yupo Mmoja tu awezaye kukupa Uzima, na Yeye atafanya hivyo. Kama utaweka Ishara kazini, usiku wa leo, Yeye yupo hapa kujitoa Mwenyewe kwako na kukupa Uzima. Yesu Kristo ndiye Uzima wako. Hivi hutampokea Yeye, usiku wa leo, tunapoinamisha vichwa vyetu?

193 Kila mtu awe na kicho, ndani na nje, katika orofa za chini na popote. Huu ni wakati makini. Huu ni wakati wa kuwa na shukrani. Huu ni wakati ambapo unamshukuru Mungu mezani pako, leo, enyi watu, natumai mlifanya hivyo, kwa ajili ya chakula ambacho Yeye alikuwa amewapa. Kitu kilichokufa, kwamba kitu fulani kilikufa ili uweze kuishi, na wewe unamshukuru Mungu kwa kukifanya kiote ili uweze kuishi kwacho.

194 Sasa, usiku wa leo, kwa nini usikubali, si uhai huo wa kimwili ambao lazima urudi ardhini pamoja na kitu kilichokufa, bali kwa nini usiukubali Uzima wa Milele, ambapo Yeye alitoa kitu, akakiinua, Mwana Wake Mwenyewe; ili uweze kugeuzwa kwa sura Yake Mwenyewe, kwa kufanywa upya roho yako, kuondoa yako na kupokea Yake, ambayo ndiyo Ishara kwamba unao Uzima. Na Yeye atapita juu yako na atakufufua kwenye siku ya ufufuo.

195 Hii ingekuwa ni kutoa shukrani kwelikweli. Hii ingeonyesha shukrani zako kwa Mungu Yule aliyefanya njia kwa ajili yako, na kuweka Uzima wa Milele mbele zako, juu ya meza Yake Mwenyewe, na anakualika kwa Huo usiku wa leo. Ungewezaje kukataa Huo? Ungewezaje kuketi kwenye meza na kushukuru kwa chakula cha kimwili, katika desturi ambayo baba zetu wasafiri walifanya, kwenye Siku ya Kutoa Shukrani; mbona si wakati huu ambapo imefanywa dhahiri sana kwako, usiku wa leo, kwa maskini njia hii rahisi ya kuihubiri?

196 Mbona usiukubali sasa, na kusema, “Ninataka Uzima wa namna hiyo, Ndugu Branham. Nitakubali huo. Yesu alikufa kwa ajili yangu. Na mimi, labda nimejiunga na kanisa, nimekuwa

na kanuni ya imani; lakini kweli kuona Uzima wa Kristo ukinidundadunda tu, mpaka ulimwengu umekufa, na Yeye akiishi Maisha Yake ndani yangu kama Yeye alivyoyaishi hapa duniani, siuoni, Ndugu Branham. Nami ninataka kuwa nao. Ninataka kuwa na hakika."

197 Huwezi kuthubutu kubahatisha. Tumechelewa mno sasa. Tunachelewa mno kwa huku kubahatisha. Hebu tupokee Huo sasa.

198 Sasa, siwezi kuwaleta watu kwenye madhabahu haya. Siwezi kufanya hivyo, hakuna nafasi ya kutosha hapa. Lakini miito ya madhabahuni ni desturi, tena. Miito ya madhabahuni ilianza katika siku za Wesley. Ile halisi, "Wote walioamini walibatizwa," Biblia ilisema.

199 Ni wangapi hapa ndani, ninaoweza kuwaona vizuri, juu kwenye roshani, huku katika ushoroba, na juu-chini kwenye kuta, na katika marefu, sijui ni wangapi walioko nje au chini katika orofa ya chini. Lakini ni wangapi wenu, wanaotaka hiyo Ishara, Roho Mtakatifu maishani mwako, ambayo itajionyesha Yenyewe moja kwa moja mbele zako? Moja kwa moja mbele za madhehebu na mambo ya ulimwengu huu, kwamba unaweza kuona kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Damu imepakwa. Hivi mnaweza kuinua mikono yenu, na kusema, "Ndugu Branham, mimi sasa, kwa kuinua mkono wangu, ninaonyesha kwa Mungu, ninataka hiyo katika maisha yangu. Niombee, Ndugu Branham."

200 Kuna mikono ishirini au zaidi, nadhani, iliyoinuliwa. Je! kuna wengine? Uinue tu. Hata nisipouona, Yeye atauona. Huko juu kabisa kwenye roshani, juu katika vyumba vyenye kioo huko juu, kama mtainua tu mikono yenu, Mungu atakuona. Huko nje, Mungu atakuona. Chini katika u—ukumbi wa orofa ya chini, Mungu atawaona ikiwa mtainua mikono yenu.

201 Ndugu, dada, sasa kwenu enyi watu ambao mmempokea Kristo miaka iliyopita, na labda unahisi kwamba—kwamba umeipokea hiyo Ishara. Natumai kwamba ni kweli. Kama umeipokea, huna haja ya kuhangaika juu yake. Hiyo hujiakisi Yenyewe. Ningewezaje kujizuia kuwa Beethoven kama aliishi ndani yangu? Ikiwa Kristo yumo ndani yako, jitazame tu katika kioo cha Mungu hapa, Biblia. Uone vile mtu fulani wa Biblia alivyoonekana, uone kama unafanana na Danieli, na Ezekieli, na Wakristo wa Kanisa la mwanzoni. Uone kama unafanana nao. Je! wewe ni wa kilimwengu? Je! unapenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu? Je! hayo yote yamekufa na ukawa kiumbe kipya?

202 Nyuma upande wangu wa kulia, nyuma kwenye pembe hapa, mwaweza kuinua mikono yenu, na kusema, "Nikumbuke mimi, Ndugu Branham, kwa kweli ninataka kuonyesha hiyo Ishara. Ninataka Hiyo maishani mwangu. Lazima niwe na Hiyo."

Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe. Wengi wenu, naam, Bwana anawaona. Mungu awabariki.

203 Laiti kungekuwa na njia fulani sasa, baada ya kuinua mikono yenu namna hiyo, na hapana shaka labda wako wengi namna hiyo kwenye orofa ya chini, karibu, kama walivyo kwenye orofa ya juu hapa, na—na kwa hiyo tunashangaa tu . . . Ninaweza kufanya nini sasa? Hapa nimeninii, nimewaambia Neno, mimi . . . katika njia rahisi niliyo nayo, kwa sababu mimi ni—mimi ni mtu rahisi tu. Na hiyo ndiyo unayotaka kuwa sasa hivi, rahisi tu. Jifanye tu rahisi. Na Mungu ni rahisi sasa.

204 Iwapo hujawahi kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, njoo. Watakubatiza, usiku wa leo, kama unataka kubatizwa. Kuwa na shukrani kwa Mungu kwamba kuna njia ya kuishi. Ulikuwa na shukrani, leo, kwamba uliishi Marekani. Shukuruni Mungu kwamba mna kanisa hapa linaloamini Neno la Mungu. Unamshukuru Mungu kwa sababu Yeye amekupa chakula ule, ili uweze kuishi muda mrefu zaidi kidogo, sasa kwa nini usimpokee Yeye na kuwa na shukrani kwa ajili ya Roho Mtakatifu anayekupa Uzima wa Milele. Kwa nini usije na kumkubali Huyo? Je! kuna mwingine ambaye hajainua mikono yao, angetaka kufanya hivyo sasa, wazi hapa hata niweze kuona? Vema. Mungu akubariki, msichana. Mungu ambariki msichana huyo. Na Mungu akubariki. Hilo, hilo ni jema.

205 Maanisha tu hiyo kwa kweli sasa, maanisha tu kwa kweli. Majira haya ya kumalizia sasa, tunazo dakika tano hadi wakati wa kumalizia, hadi saa tatu u nusu. Hebu tuketi tu kwa dakika moja, ndani na nje. Hebu tuwazie hili, kwa uaminifu. Si . . . Hiyo huleta mihemko, hakika. Lakini hebu tusiwazie mhemko hivi sasa. Hebu tuwazie uaminifu wa kile tunachofanya, "Kwa imani ninaweka mikono yangu juu ya Sadaka yangu, Yesu Krsito. Ninataka kutambulishwa katika kifo Chake. Nimemalizana na ulimwengu. Nimemalizana na Hollywood. Nimemalizana na mitindo."

206 Wanawake, "Nimemalizana na kukata nywele zangu. Nimemalizana na kuvaa nguo za kizinifu. Nimemalizana na kujipodoa. Nimemalizana na kucheza karata. Ni—nimemalizana na takataka za ulimwengu."

207 Ewe mwanamume, vivyo hivyo, "Nimemalizana na kunywa pombe. Nimemalizana na uvutaji sigara. Nimemalizana na kusema uongo. Nimemalizana na mizaha. Nimemaliza—nimemalizana na kufanya masihara. Nimemalizana na haya yote maneno yasiyo maana ambayo Biblia ilisema tutatoa hesabu kwa ajili yake."

208 "Ninataka Muhuri. Ninataka Ishara maishani mwangu. Ninaweka mikono yangu, kwa imani, sasa hivi, juu ya Sadaka yangu, Yesu Kristo. Ninajitambulisha mwenyewe kama mwanamume aliyekufa," au mwanamke aliyekufa, mvulana au

msichana. "Ninakufa sasa, pamoja na Yeye, kwa sababu Yeye alikufa ili niweze kuishi. Nami ninakubali Uzima wangu, katika Yeye. Na, Ee Bwana, ifanye ijulikane kwangu, usiku wa leo, kwamba Uzima wa Milele sasa unakaa ndani yangu."

209 Waza mawazo hayo. Amini mambo hayo. Hebu kundi hili lote la watu wanaosimama hapa, juu, chini, na kote mahali hapa, hebu wote wachukue hilo kwa kilindi na kwa uaminifu. Mtaona mkutano wa uponyaji ambao hamjawahi kuona hapo kabla, huu ukianza, huo utakapoanza. Tunachohitaji sasa ni uponyaji wa nafsi zetu, imani, ki—ki—kitu fulani ndani yetu kinachoshikilia Neno, ambacho wakati unapoona Neno limefanywa halisi. "Nena tu Neno, na Hilo litakuwa hivyo." Kama yule Mrumi alivyomwambia Yesu, "Nena tu Neno, na itakuwa hivyo."

210 Baba wa Mbinguni, ninatambua kwamba maombi yangu sasa ni kati ya walio hai na wafu. Inanibidi kusema nini, Bwana? Ni maneno ya aina gani niwezayo kutumia? Ni tamshi gani ninaloweza kuja nalo Kwako, Bwana? Sijui la kusema. Wameinua mikono yao. Unajua kilichokuwa nyuma yake, kama walimaanisha, ama kulifanya tu kama desturi, ama kama kweli walimaanisha hilo. Kama walimaanisha, Bwana, ninajua Wewe unamaanisha Neno Lako. Uko tayari kuonyesha chochote ambacho Wewe uliahidi.

211 Pia ninaombea watu hao sasa. Kila mmoja wao, ninadai kwa ajili ya I-. . . kwa ajili ya Kristo. Kila mmoja, ninadai kama kumbukumbu ya ushindi kwa ajili ya Ujumbe huu usiku wa leo, wa Damu ya Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu ambaye alitokana na Damu. Kemia, hakika, Yeye alitoa Damu Yake. Alifufua mwili Wake, bali alitoa Damu Yake. Kemikali zilikauka, muda mrefu uliopita, pale chini Kalvari. Bali Ishara iliyokuwa katika kemikali hizo, Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani ya kemikali hizo, ni mpya tu na halisi, usiku wa leo, kama alivyokuwa siku ile ambapo kemikali zilivunjwa katika mwili Wake. Hiyo ndiyo Ishara. Hiyo ndiyo Ishara, Ishara ya milele, Hiyo ni Uzima wa Milele. Ninaomba ya kwamba Hiyo itakuja juu ya kila mmoja sasa walioinamisha vichwa vyao, na kama watapokea Hiyo.

212 Wana shukrani, usiku wa leo, Bwana, kwamba Wewe ulifanya njia. Wana shukrani kwa ajili ya Yesu Kristo, bidhaa iliyokufa ambayo Wewe ulifufua kwa ajili ya kutuhesabia haki, kuonyesha ya kwamba tukichukua kutoka kwa Uhai Wake, tunaweza kuishi milele. Jalia Huo uje juu ya kundi hili, hao walioinua mikono yao. Na labda baadhi yao, wakijua walipaswa kuwa wamefanya hivyo, bali wameiweka kando muda mrefu sana, na muda mrefu, mpaka baada ya kitambo kuna kovu limekatwa hapo. Hakuna shauku tena. Mungu, mtikise mtu huyo tena. Huu huenda ikawa ndio usiku wa mwisho duniani ambao wataishi. Kesho huenda ikawa imechelewa sana.

213 Bw. Kennedy alijuaje, kwamba akiteremka barabarani, akicheka, kwamba katika dakika moja zaidi, angekuwa analala pajani mwa mkewe, amekufa. Juma lililopita alikuwa na furaha, akishangilia, akicheza na watoto wake, usiku wa leo mwili wake unaozea kaburini. Mtu maarufu, Rais wetu, ila kifo hakipendelei yeyote. Hakina budi kuja.

214 Na sasa, Bwana, jalia tujiandae kwa kifo hicho katika saa hii. Ninaikubali, Bwana, upya. Nina shauku ya kujiweka upya na Wewe, usiku wa leo, Bwana, ninaposimama mimbarani. Kama nilivyowazungumzia watu asubuhi ya leo, kuhusu kuzuriwa na Wewe juu ya mlima, Bwana Mungu, ni—ninakuahidi Wewe, upya, jalia niishi mradi tu Wewe unanitaka mimi niishi, na unijalie niwe mkweli kwa kanuni za Neno hili. Jalia niishi hivi, hata ninaweza kutupilia mbali mawazo yangu mwenyewe, nitupilie mbali maisha yangu mwenyewe, na kuacha Maisha ya Yesu Kristo kujiakisi kupitia hayo, katika Neno Lake lililoahidiwa la siku hii. Pia jalia ahadi hii kuu ije juu ya kila mtu aliyepo sasa, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo.

215 Huku tumeinamisha vichwa vyetu sasa.

> Kuna chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa katika mishipa ya Imanueli,
> Na wenye dhambi wakitumbukia chini ya gharika hilo,
> Hupoteza waa lao lote la hatia,
> Hupoteza waa lao lote la hatia,
> Hupoteza waa lao lote la hatia,
> Na wenye dhambi wakitumbukia chini ya gharika hilo,
> Hupoteza waa lao lote la hatia.

216 Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu. Nyinyi mliofanya hilo, kumkubali, "Yesu Kristo, ninakutaka Wewe. Ninaitaka Ishara Yako." Unaona, ni maombi yako ndiyo yanayokuokoa, ni imani yako ndiyo hukuokoa. Je! unaamini sasa kwa moyo wako wote, na uko tayari kwa ubatizo wa Kikristo, hivi unaweza tu kuinua mkono wako? Sema tu, "Niko tayari." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Kwenye orofa ya chini, sijui ni wangapi wako huko chini. Mwahidi tu Mungu. Nyuma pembeni hapa, upande wangu wa kulia. "Sasa ninamwamini Yesu Kristo, na niko tayari kwa ubatizo wa Kikristo."

217 "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi." Kwa kusudi gani? Unabatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa kusudi gani? Kwa ondoleo; kuondoa! "Hakuna jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu." Kwa ondoleo la dhambi! "Nanyi mtapokea Ishara. Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu."

218 Na kama Mungu akikuita, na wewe uliinua mkono wako, basi ahadi ni kwako wewe. Kuwa na shukrani. Jitayarishe hapa juu na kujitambulisha na Kristo, huku unapokuja kwa ubatizo wa maji. Mhudumu atakutana na wewe hapa na kuandaa kwa ajili ya ibada za ubatizo, unapotaka kubatizwa. Nadhani wanayo mavazi na kadhalika tayari hivi sasa, katika orofa ya chini, kwa ajili ya ibada ya ubatizo, kama unataka hivyo. Usiahirishe, kesho. Ifanye sasa. "Yeye awekaye mkono wake kwenye jembe la ng'ombe, na hata anageuka kutazama nyuma, hastahili kulima na jembe la ng'ombe." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Iweke Ishara hadharani mahali pako pa kazi. Wewe weka Hiyo hadharani, kila mahali. Ama, kama mna shukrani, inueni mikono yenu, na shukrani kwa Mungu, kwamba umetambulishwa na Kristo. Mungu awabariki. Naam.

219 Sasa, dada kwenye kinanda, *Imani Yangu Yakutazama Wewe*. Dada Anna Jeanne, kama utaambatana naye kwenye piano. *Imani Yangu Yakutazama Wewe*, huku tukisimama, pia, juu kwa miguu yetu sasa, kutoa ushuhuda kwa Mungu. Hebu kila mmoja wetu sasa, tuimbe wimbo huu wa kale wa kanisa, kwa siku za usoni, kwamba tukiondoka hapa, ulimwengu huu, kabla ya Shukrani ijayo tena, siku ya Kutoa Shukrani, kwamba kila siku katika maisha yetu itakuwa ni kutoa shukrani, kwamba Neno lingali hai, hata tunatambulishwa na Yeye, katika mauti, kuzikwa, na kufufuka.

220 Na sasa nyinyi kwenye orofa ya chini, nyinyi juu kwenye roshani, na nyinyi mlio nje, katika ushoroba, mtu fulani atakutana nanyi hapa sasa, kuchukua ombi lenu kwa ajili ya ubatizo wa maji, kwa kitambo kidogo tu.

221 Hebu tufumbe macho yetu sasa, tuinue mikono yetu, kwa ajili ya sadaka yetu ya kutolea shukrani kwa Mungu, orofa ya chini, orofa ya juu, kila mahali. Vema.

Imani yangu yakutazama Wewe,
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Ee Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Wala usiniache da-. . .
Tangu leo niwe Wako kabisa!

Wakati ninapotembea katika mzingile wa maisha yenye giza, (kuwa nuru)
Na huzuni imenizunguka kote, (onyesha Ishara yako)
Uwe Kiongozi wangu Wewe;
Amuru giza ligeuke kuwa mchana,
Loo, yapangusie mbali hofu zangu zote,
Wala usiniache nitangatange
Kutoka Kwako kwenda kando.

222 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, "*Imani Yangu Yakutazama Wewe*." Ndugu fulani anaanza kunena katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu huyo anaendelea kunena katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu fulani anatoa tafsiri—Mh.]

223 Iweni tu na kicho kabisa. Pamoja na mwito kama huo, ninajihisi kwamba ninapaswa kuwaita hao watarajiwa kuja hapa juu mbele ya madhabahu haya. Je! imani yako inatazamia hiyo? Mnakumbuka wakati mmoja kusanyiko lilipokuwa linasimama, ndipo Roho akamshukia mtu mmoja naye akatabiri. Kunena kwa lugha, na tafsiri, ni unabii. Kwa hiyo, ninawauliza wale watarajiwa sasa, kama mtakuja mbele, nyinyi msiojua hakika ya kwamba mnayo Hii. Je! mlisikia onyo hilo? Hamna muda mwingi zaidi. Huenda kukawa nafasi yako ya mwisho, usiku wa leo, huenda ukamhuzunisha Huyo kwa mara ya mwisho.

224 Naomba mje, huku tukiendelea kuinamisha vichwa vyetu. Na tuimbe tena, kwa sauti ya chini, "Kuna chemchemi" (lisahihishe, hapa sasa) "iliyojaa Damu, iliyotolewa kwa mishipa ya Imanueli." Vema. Huku mmeinamisha vichwa vyenu. Njoni, watarajiwa. Ninataka ku . . . Mungu awabariki. Njoni moja kwa moja huku juu sasa, orofa ya juu; au, orofa ya chini, pandeni juu na mjikusanye pamoja, na kutuma mhudumu huko chini sasa kulishughulikia. Njoni mbele sasa. Nyinyi mnaokuja, pandeni juu sasa hivi. Usiliahirishe tena. Usimruhusu Shetani aseme, "Loo, wakati mwingine." Lifanye sasa hivi. Sasa hivi, upesi, songa. Ishike fimbo yako mkononi mwako. Fimbo mkononi mwako, viuno vyako vimefungwa; pasaka inakuja.

> . . . waa la hatia.
> Hupoteza waa lao lote la hatia,
> Hupoteza waa lao lote la hatia.

225 Endeleeni tu kuja, njoni moja kwa moja chini, njoni moja kwa moja huku karibu.

> Na—na wenye dhambi wakitumbukia . . .

226 Usijaribu, usibahatishe tu. Muda umeenda sana kwa ajili ya kubahatisha, rafiki. Kama huna hakika, njoo sasa. Sasa ndiyo wakati.

> Mwivi anayekufa alifurahia kuona
> Chemchemi hiyo (loo, shukrani halisi!) . . . siku
> yake;

227 Mtu fulani ana shukrani kwamba Mungu alimtuma Mwana Wake ili Yeye aweze kutambulishwa na watu.

> . . . mwovu kama yeye,
> Iliosha dhambi yangu yote . . .

228 Mpisheni huyo mama kwenye marefu. Hiyo ni kweli. Njoo moja kwa moja, dada.

Nioshe dhambi yangu yote,
Nioshe yote...(loo, ni wakati wa jinsi gani sasa!)...mbali;
Loo, na hapo naomba mimi, japo ni mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote...

229 Loo, Chemchemi ipo hapa sasa. Hebu tuinue mikono yetu, kila mahali, kwa kutoa shukrani kwa Mungu. Kutoa shukrani!

230 Baba Mungu, pokea shukrani zetu, usiku wa leo. Wapokee watu hawa katika Ufalme Wako, Bwana. Tunakupa Wewe shukrani na sifa, kupitia Bwana wetu Yesu.

231 Baadhi yenu ndugu shukeni mwende miongoni mwa watu hawa sasa. Njoni moja kwa moja miongoni mwa watu.

232 Mungu asifiwe! Nina shukrani, usiku wa leo, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, na kwa ajili ya mambo tunayojua kwamba Yeye anafanya.

233 Nyinyi mlio karibu na madhabahu sasa, salimisheni maisha yenu moja kwa moja Kwake. Hebu huu uwe ndio wakati ambapo kwamba Uzima unaingia ndani.

Hupoteza waa lao lote la hatia.

234 Kuwa tu na shukrani kwa Bwana sasa, kila mmoja wenu, kwa shukrani tu. Yeye alikuahidi Roho Mtakatifu; shukuru kwa ajili Yake. Hilo ndilo walilokuwa wakifanya, kumshukuru na kumbariki Mungu, kwa ajili ya ahadi. Amini tu hilo sasa!

Ndugu Don, njoo.

*Ile Ishara* SWA63-1128E

(The Token)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 28 Novemba, 1963, katika Maskani ya Life kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org